

# *YEHOVA-YIRE* <sup>1</sup>

 Na tuendelee kusimama tu kwa muda kidogo wakati tumeinamisha vichwa vyetu kwa maombi. Tunapoinamisha vichwa vyetu, sijui ni wangapi usiku huu wangetaka kukumbukwa katika maombi, una jambo fulani moyoni mwako unalotaka Mungu akufanyie, inueni tu mikono yenu. Bwana na awajalie haja hizi sasa tunapoinamisha vichwa vyetu na mioyo yetu mbele Zake.

<sup>2</sup> Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia Kiti Chako cha Neema tena, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana mkuu wa Mungu. Tunakushukuru kwa fursa ya kuja na hakikisho ya kwamba Wewe utasikia na kujibu tunayoomba. Tunaomba, Baba, ya kwamba utasamehe dhambi zetu, yaani, kutokuamini kwetu. Na, Baba, tunaomba ya kwamba utatupa imani, imani nyingi mno usiku wa leo. Nawe unajua kilichokuwa nyuma ya kila mkono pale, ndani moyoni. Walihitaji jambo fulani, Bwana. Waliinua mikono yao kwa uchaji, wakitarajia kitu kutoka Kwako. Nami ninaomba, Baba wa Mbinguni, hata kiwe kilikuwa ni nini, kwamba watu hawa watapewa.

<sup>3</sup> Tunakushukuru kwa kutuzuru jana jioni. Tunaomba kwamba utarudi kwetu pamoja na nguvu na neema nyingi usiku wa leo, na utatujalia haja za moyo wetu, kwa kuwa, kwa hakika shauku yetu ni kufanya Mapenzi Yako na kuona Mapenzi Yako yakinende. Nasi tunajua Mapenzi Yako ni nini kuhusu wagonjwa, kwamba ulipigwa mgongoni Mwako kwa uponyaji wetu, "Kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa." Na, Baba, tunaomba kwamba—kwamba Mapenzi yako makuu yatafanyika usiku wa leo, kutupa imani kuamini hivyo, kwa wingi, kusudi kila mgonjwa aponywe, na kila mtu aliye potea akumbuke ya kwamba Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu. Tujalie, Bwana.

<sup>4</sup> Jalia wajue ya kwamba mradi tu kuna Dhabihu iliyoojaada—damu Pale kwa ajili yao, dhambi zao haziwezi kuonekana kwa Mungu. Bali kama wakifa bila kuitubia Hiyo hadharani na kuikubali, na kuzaliwa mara ya pili, kamwe kusingekuwako na njia hata kidogo kwao kuingia kwenye ule Ufalme. Pia jalia huu uwe ndio usiku ambao kila mtu asiye chini ya ile Damu aingie haraka chini Ya hiyo Damu usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu. Nasi tutakupa sifa. Amina.

<sup>5</sup> Majaliwa makubwa sana kuwa hapa usiku wa leo na kuzungumza tena. Na jana jioni tulikuwa na wakati mzuri sana, kuzuriwa na Bwana. Ila niliwachelewesha sana. Kamwe siwezi kumalizia kwa wakati mzuri, kwa namna fulani.

<sup>6</sup> Kwa namna fulani karibu nipate juu jingi kupita kiasi leo. Nilikuwa . . . Mwanangu mdogo, Joseph, amekuwa akinisihi aende akaogelee. Kwa hiyo mahali tunapokaa pana kidimbwi kidogo, kwa namna fulani kimejengewa ua kule nyuma, naye akasema, “Njoo, niangalie, baba. Ninaweza kuogelea.”

Nikasema, “Sawa.”

<sup>7</sup> Nilishuka nikaenda pale asubuhi ya leo, nikachukua Biblia yangu, na ninii . . . kuandika mihtasari fulani. Na wakati nilipokuwa nikisoma, yeye . . . huyu hapa anakuja amevaa kaptura ya kuogelea, akasema, “Hebu niangalie, baba, ninaweza kupiga mbizi!” Vema, kama niliwahi kumwona chura akiruka majini! Ndipo akaamka, nayo maji yalikuwa yakifoka kutoka puani na mdomoni mwake, akasema, “Nilifanyaje?”

Nikasema, “Unafanya vema.”

<sup>8</sup> Ndipo nikaanza kuwazia juu ya wakati mmoja nilipomwambia baba yangu jambo lile lile. Kidimbwi kidogo cha zamani, kabla hatujafika mtoni, kulikuwako na kidimbwi, nasi watoto wadogo kwa kweli ilitubidi tuondolee mbali taka za juu kutoka kwake, nasi tungeninii . . . maji hayo hayakuwa na kina cha zaidi ya inchi sita. Nami nilishikilia kumwambia baba yangu, “Ninaweza kuogelea.”

<sup>9</sup> Kwa hiyo Jumapili moja alasiri alienda pale. Nao walikuwa na kijisanduku kidogo cha sabuni kimewekwa pale. Ndipo nikaenda nyuma kichakani na kuvua nguo zangu, chochote kilichokuwako cha kuvua; ninavuta tu pini moja, wajua. Na ni wangapi waliopata kuona moja kama hiyo? Sawa. Jozi tu ya ovaroli, bila mikanda; i—imefungwa tu na kamba ya nyasi kavu, badala ya mikanda, halafu ni pini tu. Unaivuta pini hiyo na, hivyo ndivyo tu inavyokubidi kufanya, unaruka ndani mara moja. Na kwa hiyo nikapanda juu ya kijisanduku hiki na kuziba pua yangu, unajua, na kujitumbukiza humo, nayo matope yakaruka juu umbali *huo*. Baba yangu ameketi pale chini, akiniangalia. Nikasema, “Unanionaje?”

<sup>10</sup> Akasema, “Toka humo uende ukaoge!” Nilikuwa nikiwazia hilo liliendelea kwa muda gani!

<sup>11</sup> Na, unajua, wakati unatukimbia kabisa, sivyo? Inavyoonekana, kamwe hatuna wakati, tena, wa kufanya mambo. Wala muda haumngojei mtu yeyote. Kwa hiyo hatuna budi kufanya kazi tuwezapu, kwa kuwa saa yaja wakati kizazi hiki kitaondoka, na kutakuwako na kizazi kingine kitakachokuja, kama kuna na kizazi kingine. Hakika, ninasema kwa moyo wangu wote, (sijui ni wakati gani atakapokuja; hakuna mmoja wetu ajuaye), lakini, hakika, sidhani kutakuwako na kizazi kingine. Ninaamini Kristo atakuja katika kizazi hiki. Sijui ni wakati gani, sasa, huenda ikawa ni usiku wa leo ama huenda ikawa ni miaka kumi tangu sasa, ama ishirini, bali ninaamini atakuja katika kizazi hiki. Ninaamini jambo hilo.

Asipokuja, ninataka kuishi kana kwamba tu anakuja, hata hivyo, maana ninajua kwamba huenda ikawa ndiyo siku yangu ya mwisho, ama siku yako ya mwisho.

<sup>12</sup> Halafu basi, kumbukeni, kama tukiondoka kabla hajaja, tutapaa juu na katika Uwepo Wake, ama, tutafufuliwa kabla wengine hawajabadilishwa. "Parapanda ya Bwana italia, waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai na tuliosalia tutabdalishwa kwa dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na kunyakuliwa pamoja nao, kumlaki Bwana hewani." Angalieni utaratibu wa ufufuo. Mnaona, Mungu anajua ya kwamba tunatamani kuwaona wapendwa wetu. Na kama tulifika kule kumlaki Yeye kwanza, tutakuwa tukiangalia huku na huko tuone kama mama ama baba na hao wengine walikuwako. Bali mnaona jinsi ambavyo, Roho Mtakatifu katika hekima Yake? Tunakutana sisi kwa sisi kwanza, kisha tutakapofika kule na kuimba *Neema ya Ajabu*, hapo ndipo kutakuwako na wakati wa kuabudu. Mnafikiri ninachekesha sasa, hebu mniangalie Kule juu! Utakuwa ni wakati mzuri sana kwangu mimi na sisi sote tutakapofika Kule.

<sup>13</sup> Sasa hebu tusome baadhi kutoka kwenye Biblia hii ya kale iliyobarikiwa hapa usiku wa leo. Hebu na tufungue kwenye Warumi, mlango wa 4, na tusome sehemu moja tu kutoka katika Kitabu cha Warumi. Ninataka kusoma katika sehemu mbili usiku wa leo, kutoka katika Mwanzo na kutoka katika Kitabu cha Warumi. Sasa katika Kitabu cha Warumi, mlango wa 4, kifungu cha 17.

*(Kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi,) mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, anayewahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako.*

*Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi, kama ilivyoandikwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

*Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, hakufikiria hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, (akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia), wala... hali ya kufa ya tumbo lake Sara.*

*Lakini akiiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu;*

*Huku akijua hakika ya kuwa Mungu aweza kufanya yale aliyoahidi.*

*Kwa hiyo iliheabiwa kwake kuwa ni haki.*  
*Walakini haikuandikwa kwa ajili yake tu kwamba iliheabiwa kwake;*

*Bali ni kwa ajili yetu sisi tunaomwamini yeye  
aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu;*

*Ambaye alitolewa kwa ajili ya makosa yetu, na  
kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki.*

<sup>14</sup> Loo, jinsi ninavyoyapenda Hayo! Hapo ni sehemu mojawapo ya Maandiko ninayopenda sana kusoma katika Biblia, kwa sababu ni dhahiri sana kile Mungu alichokuwa, yale aliyoahidi na kuapa kwamba atatimiza. Na sasa nililichagua somo hili kwa sababu ninawazia kwamba katika mukutano wowote, kuona imani tuliyonna ikitumiwa hapa jana usiku, hata hakuna mtu mnyonge mmoja mionganoni mwetu ambaye hakuponywa. Jinsi nguvu za Mungu zilivyokuja na yale Yeye aliyofanya! Ndipo nikawazia, kama tungeweza kujenga juu ya kitu kilicho dhahiri, tukilenga ku—kufanikiwa, basi lingekuwa ni jambo zuri jinsi gani wakati tungeweza kuufikia usiku huo mkuu ama wakati wa kipeo.

<sup>15</sup> Pia hatuna budi kukumbuka ya kwamba hakuna jambo linaloweza kufanyika bila ya imani, na kwanza lazima iungamwe. Kwa kuwa Yeye ndiye—Yeye ndiye Mwanzilishi wa imani, tunajua hilo, na kwamba hakuna jambo liwezalo kufanywa pasipo imani. Na bila ya imani haiwezekani kumpendeza Mungu.

<sup>16</sup> Na sasa Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Sasa ya—ya Mfalme James hapa, katika Kitabu cha Waebrania, inasema “kukiri.” *Kukiri na kuungama* ni kitu kile kile, kukiri na kuungama. *Kukiri linamaanisha* “*kusema jambo lile lile*”: “Kwa mapigo Yake nimeponywa,” unaona, “Sasa kwa Uzima Wake nimeokolewa.” Na sasa basi, kwanza, hatuna budi kukiri jambo hilo; Naye ameketi kama Mpatanishi, na Mpatanishi pekee kati ya Mungu na mwanadamu, Naye ameketi pale kuombea yale tunayokiri kwamba Yeye amefanya. Hilo ni ja—jambo dhahiri, halisi jinsi gani!

<sup>17</sup> Na sasa ninataka kusoma Andiko lingine, linalopatikana katika Kitabu cha—cha Mwanzo, mlango wa 22, na hebu tuanzie kusoma hapa kwenye kifungu cha 7.

*Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena,  
Babangu! Naye akasema, Mimi hapa, mwanangu.  
Akasema, Tazama! Moto upo, na kuni zipo, lakini yuko  
wapi mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa?*

*Ibrahimu akasema, Mungu atajipatia mwana-kondoo  
kwa hiyo sadaka, mwanangu. Basi wakaendelea wote  
wawili pamoja.*

*Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu,  
Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari  
kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka  
juu—juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.*

*Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe.*

*Ndipo malaika wa BWANA akamwita kutoka mbinguni akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa.*

*Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno, kwa maana sasa ninajua ya kuwa—ya kuwa unamcha Mungu, na kuona wewe... hukunizuilia mwanaao, mwanaao wa pekee.*

*Ibrahimu akainua macho yake... na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaahuyu kondoo, akamtoa juu ya... awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanaawe.*

*Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-Yire, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana.*

<sup>18</sup> Somo lile ningetaka kutoa hapo, kama lingbeitwa somo, *Yehova-Yire*, neno hilo linamaanisha “Bwana atajipatia Mwenyewe dhabihu.” Kama hana moja, anawenza kujipatia moja. Ninashukuru sana kwa jambo hilo. Sasa somo hili kuu! Na sasa tukisoma pale, ya kwamba “Ibrahimu hakusita kwenye ile ahadi kwa kutokuamini; bali alitiwa nguvu, akimtukuza Mungu.”

<sup>19</sup> Sasa, Ibrahimu ndiye ambaye Mungu alifanya agano naye na kumpa ahadi; na Ibrahimu, si yeze tu, bali Uzao wake baada yake, “Ibrahimu na Uzao wake.” Na sasa kumbukeni jambo hili sasa. Kama tumekufa katika Kristo, sisi ni Uzao wa Ibrahimu kama tumezaliwa mara ya pili. Sasa, hebu tuwe waangalifu sana kuhusu jambo hili sasa tunapolichunguza somo hili. Na sasa kama mtasikiliza kwa makini, nina hakika Roho Mtakatifu atawafunulua. Mtalishika lile tumaini, nalo litautia mwanga mji huu na kila kitu karibu nawe, kama tu tukiuchukua wakati wetu na kulishika lile wazo, kile Roho Mtakatifu anachojaribu kutufahamisha. Sasa, Ibrahimu, aliita, kile kilichoitoa hiyo ahadi, kwa Ibrahimu na Uzao wake.

<sup>20</sup> Sasa kuna mengi sana leo, enyi marafiki, yanayoitwa Ukristo, ambayo sio Ukristo.

<sup>21</sup> Sasa, ninachukia tu kusema jambo hili. Lakini ni afadhali nisimame hapa na niwe ninapendwa sana mionganii mwa watu, na—na kila mtu akikupigapiga mgongoni mwako, na kila kitu namna hiyo. Lakini basi sina budi kukutana na kundi hilo kwenye ile Hukumu, kutoa hesabu kwa ajili yake. Kwa hiyo i—inanibidi tu kuwa mwaminifu.

<sup>22</sup> Sasa tunaweza kuyaangalia makusanyiko, na juu ya ulimwengu siku hizi, juu ya kile kinachoitwa Ukristo, na kuona kwamba uko maili milioni moja kutoka kwenye

Ukristo. Na imebashiriwa katika Biblia kuwa hivyo. Sasa wengi wanamkulali Kristo katika njia ya kusema, "Vema, ninamwamini." Mbona, ibilisi anaamini jambo lile lile. Unaona? Na wengi wao wanajaribu kulikubali juu ya mhemuko, kusema, "Vema, nilinena kwa lugha. Nilicheza katika Roho." Nimewaona wachawi wakifanya jambo lile lile, na wacheza dansi za ibilisi huko Afrika; hakika, wakinena kwa lugha, na kunywa damu kutoka kwenye fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita ibilisi. Mama yangu ni Mhindi, nusu Mhindi, na—na watu wake. Nimewaona wakiichukua penseli na kuiweka chini namna *hiyo*, na kuiona penseli ikitisogea na kuandika katika lugha zisizojulikana, wao wanasmama pale na kuzifasiri, wakimwita ibilisi. Hakika. Unaona, huwezi kuongozwa na mihemuko. Unaona, maisha yako unayoishi yanashuhudia wewe ni nani. Unaona? Haidhuru ni mhemuko wa jinsi gani, huwezi kuuwekeea Ukristo msingi juu ya mhemuko.

<sup>23</sup> Ni maisha! Yesu alisema, "Kwa tunda lao mtawatambua." Si kwa maungamo yao, sio kwa yale wanayosema. Na Yesu pia alisema, "Mnanijia kwa midomo yenu, bali moyo wenu uko mbali na Mimi." Hayo, hayo ndiyo maungamo yao. Unaona, maisha yako yanakutambulisha. Na kama mtu akisema ya kwamba anamwamini Mungu, na anakana Neno moja la Biblia hii, ama anaibadilisha kwa njia yoyote, basi haina budi kuwa ni kosa.

<sup>24</sup> Mnasema, "Haileti tofauti yoyote kuhusu mambo haya madogomadogo." Hakika inaleta tofauti.

<sup>25</sup> Neno moja dogo ndilo lililotuingiza katika shida hii yote; sio kutoliamini, bali ni kuliweka tu mahali pengine. Hawa alikoseshwa tu na Shetani, akampa tu hoja. Huko chini kwa Ndugu Williams, ndio kwanza nimalize kupitia hayo huko Santa Maria. Hicho ndicho kitu kilichotutoa kwenye Bustani ya Edeni, na kusababisha kila mtoto mgonjwa. Kama vile, nilivyomwombea mtoto mdogo mwenye kifafa aliylala pale, dakika chache zilizopita, wakati nikiingia. Ni kitu gani kilichosababisha jambo hilo? Kwa kuwa Hawa kamwe hakulishuku, bali alichukua tu hoja fulani, ya kwamba ni kweli hili lingekuwa ni sawa. Nalo likasababisha kila mauti, kila maradhi, kila huzuni, kila huzuni ya moyoni. Nasi tutarudi mle jinsi gani? Kama liliساببisha—kama liliساببisha miaka elfu sita ya jambo hili, tutarudie na chochote pungufu ya kila Neno kamilifu jinsi lilivyoandikwa?

<sup>26</sup> Ibilisi alishinda vita juu ya jamii ya binadamu kwa kuhojiana na jamii ya binadamu. Kuhoji tu, "Mbona, ni wazi *hili* lingetukia? Ni wazi." Kama hoja ni kinyume cha Neno, basi hiyo hoja si sahihi! Neno ni kweli, jinsi tu lilivyoandikwa! Usiweke tafsiri yoyote ya kibinagsi. Liseme tu jinsi lilivyoandikwa, na uliamini jinsi hiyo. Unaona? Mungu amelilinda. Liko tu

jinsi hasa linavyopaswa kuwa, kwa hiyo hebu na tuliamini tu jinsi hiyo.

<sup>27</sup> Sasa, ni Neno, kila Neno! Kila...Roho Mtakatifu katika mwanadamu; kila sentensi ya Biblia, Roho Mtakatifu aliye ndani yako ataliitikia kwa "amina," kwa maana Roho Mtakatifu aliiandika Biblia. Na kama yumo ndani yako, anawezaje kusema, "Vema, Hilo lilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine, Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya *huu*, ama Hilo lilikuwa ni kwa ajili ya *ule*"? Anawezaje kusema hivyo na awe ni Roho Mtakatifu ndani yako? Hawezi kusema hivyo. Inambidi kusema "amina" Kwalo!

<sup>28</sup> Sasa, kama nilivyosema hivi majuzi, jambo la kwanza ambalo Mungu aliwapa watu Wake, kuwakinga, lilikuwa ni Neno. Wala kamwe hajabadijika. Hawezi kubadilika. Sasa, kanuni za imani hazitafaa kitu, madhehebu hayatafaa kitu, elimu haitafaa kitu, hakuna moja ya mambo haya, kila moja la hayo limeshindwa kabisa na litashindwa. Kuna kitu kimoja tu kitakachofanya kazi, hicho ni Neno.

<sup>29</sup> Na jinsi tu tunavyoweza kulijia Neno, ni kwa ile Damu. Mahali pekee ambapo mtu yejote alipata kumwabudu nayo Mungu, ilibidi aje chini ya ile Damu. Hakuna matayarisho mengine kamwe. Huwezi kuja chini ya jina la Methodisti, huwezi kuja chini ya jina la Pentekoste, huwezi kuja chini ya jina la Katoliki. Kuna dazeni kadhaa za makanisa ya Katoliki, mbalimbali, yanayotofautiana, ya Orthodoxi, na Kiyunani, na Kirumi, nayo yamevunjika-vunjika sana kama ya Kiprotestanti. Waprotestanti, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Kilutheri, Katoliki, loo, kila moja, yote ni tofauti. Nayo hayo hapo, unaona. Bali kuna msingi mmoja wa ushirika, huo ni chini ya ile Damu! Nayo Damu ni Uzima, nayo daima itakubaliana na Neno, daima pamoja na Neno.

<sup>30</sup> Sasa, tunajua ya kwamba uhai umo katika jinsia ya kiume, umo katika damu, himoglobini. Kwa njia hiyo kuku anawenza akataga yai, bali endapo hajakutana na ndege wa kiume, hilo yai kamwe halitaanguliwa. Hakika, halijarutubishwa. Hivyo ndivyo nilivyoninii, nilivyotoa yale matamshi mengi makorofii, nikisema ndege jike anawenza akataga mayai kiota kizima, naye anawenza kuwa mwaminifu kwayo apendavyo kuwa, anawenza kuyalalia, na kwa mabawa yake, na kuyageuza kila dakika chache ili kuhakikisha yataanguliwa. Naye—naye ataona njaa sana, na kufunga, wakati akiwa kwenye hicho kiota, akiyashughulikia mayai hayo, hata adhoofike sana hata asiweze kuruka kutoka kwenye hicho kiota. Kama hakukutana na ndege wa kiume, na hayo mayai yamerutubishwa, yatacaa papo hapo kwenye kiota na kuoza kama hakuwa pamoja na mwenziwe. Hiyo ni kweli kabisa.

<sup>31</sup> Na hivyo ni kama vile makanisa yetu yamekuwa, yalichukua tu kundi chini ya maungamo baridi ya kawaida, dansi fulani la ajabuajabu ama mhemuko fulani. Nao wanafanya nini? Wanalishuku Neno, mpaka tukawa na kiota kilichojaa mayai yaliyooza. Wakati umewadnia wa kukisafisha kiota hicho na kuanza tena. Mpaka watakapokutana na yule Mwanamume, Kristo Yesu, na kuzaliwa tena kwa Neno. Basi hayana budi kuanguliwa, kwa maana ni Uzima.

<sup>32</sup> Wakati fulani uliopita nilikuwa nikila chakula cha jioni pamoja na mhububiri m—mzee wa Kimethodisti, nami nikasikiliza Kipindi cha Kilimo kikitangazwa kutoka—kutoka Louisville, Klabu cha 4-H kilikuwa kikizungumza, ya kwamba “Walikuwa na mashine ambayo ingetoa punje ya mahindi kama ile tu wanayokuza shambani.” Wakasema, “Ingetengeneza fleki za mahindi za namna ile ile, ugali ule ule, yalikuwa ni mahindi yale yale. Ukiyakata namna hiyo, uyaweke chini ya mwanga, uyapeleke kwenye maabara; kiini chake kiko mahali pake, na kila kitu, na kiasi kile kile cha unyevu, kalisi, potashi, chochote kilicho ndani ya mahindi hayo kimekaa vizuri kabisa.” Wakasema, “Kama ukiwahi kuchota konzi moja kutoka kwenye gunia la yale yaliyolimwa shambani, na kwenye gunia la yale yanayotengenezwa na mtambo huo, ama yaliyotengenezwa, na kuyachanganya, kamwe usingeweza kujua tofauti yake kwa jicho lako la kawaida, ama ukiyakata vipande viwili, wala sayansi yoyote isingaliweza kupata tofauti yake. Jinsi tu ungaliweza kuyatofautisha ilikuwa ni kuyazika.” Hilo linayatofautisha.

<sup>33</sup> Mtu anaweza kuonekana kana kwamba ni Mkristo, anaweza akatenda kama Mkristo, anaweza kumwiga Mkristo. Bali asipokuwa na ile chembechembe ya Uzima mle ndani, hawezি kufufuka tena; inampasa kuwa na hiyo chembechembe ya Uzima mle ndani, kuwa na Uzima wa Milele.

<sup>34</sup> Na mtu ye yeyote aliyesoma Kiyunani, anajua ya kwamba hilo “Milele” linatokana na neno Zoe, ambalo linamaanisha “Uzima wa Mungu Mwenyewe,” ambapo mtu unakuwa sehemu Yake; kama vile ulivyo sehemu ya baba yako. Unakuwa sehemu ya Mungu. Na Uzima wa Mungu Mwenyewe unatenganishwa na kuwekwa ndani yako, wala hauwezi kufa, kwa maana ni wa Milele. Chochote kilicho na mwanzo, kina mwisho; bali Yeye kamwe hakuanza, kwa hiyo hawezи kuwa na mwisho. Yeye ni wa Milele, nawe u wa Milele pamoja Naye. Huwezi kufa kama tu vile Yeye asivyoweza kufa, kwa maana unakuwa u sehemu Yake. Umezaliwa Naye. Amina. Ninaendelea tu kuzungumza juu ya jambo hilo, nami kamwe sitalifikia somo hili.

<sup>35</sup> Loo, nina furaha sana kuwa Mkristo! Mimi—mimi—mimi—mimi nisingeweza kubadilishana mahali na mtu ye yeyote ulimwenguni, sio marais, wafalme. Kama wangenipa ulimwengu mzima, waseme ningeweza kuishi miaka milioni moja; baada

ya hiyo nitakufa, baada ya hiyo miaka milioni moja. Lakini sasa, miaka milioni moja, mbona, sitakuwa chochote sasa, tunaendelea tu kuishi, hakuna mauti. Kwa hiyo ni jambo kuu kuwa Mkristo.

<sup>36</sup> Nilikuwa nikizungumza juu ya Ibrahim! Hebu na turudi nyuma. Sasa sisi ni Uzao wa Ibrahim kama tuko ndani ya Kristo. Na basi kama wewe ni Uzao wa Ibrahim, una imani ile ile aliyokuwa nayo Ibrahim, maana ilikuwa ni imani yake ndiyo tunayozungumzia habari zake. Hasa sana kanisani sasa, ni Uzao wa Kifalme wa Ibrahim. Kulikuwa na wazao wawili wa Ibrahim. Mmoja ulikuwa ni wa kawaida, Isaka; Huo mwингine ulikuwa Kristo, ile ahadi. Kwa hiyo kwa njia ya Isaka, Israeli walibarikiwa; kwa njia ya Kristo, ye ye alifanyika baba wa mataifa. Unaona? Kwa hiyo ule Uzao wa kifalme, ni jinsi gani ungekuwa ni mkuu kuliko ule uzao wa kawaida wa Ibrahim. Kwa hiyo kama wewe uko ndani ya Kristo, wewe una Uzao bora kabisa, wa juu zaidi ukilinganisha na jinsi Ibrahim aliivyokuwa, kwa maana umetokana na Uzao wa kifalme, Kristo. Kama mmekufa katika Kristo, basi ninyi ni watoto wa Ibrahim, nanyi mna Uzao wa Ibrahim na imani ya Ibrahim. Nayo imani ya Ibrahim ilikuwa katika Neno la Mungu haidhuru ni jambo lipi lililotukia. Aliyaita mambo yale yasiyokuwako kana kwamba yalikuwako, kwa kuwa Mungu alisema hivyo. Ni ahadi ya jinsi gani!

<sup>37</sup> Sasa hebu na turudi nyuma kidogo na kuwekea msingi mawazo yetu. Hebu na turudi nyuma, kabla hatujafika kwa Yehova-Yire, kwa Ibrahim. Hebu turejee nyuma, turudi nyuma kidogo katika Maandiko. Hebu turudi kwenye mlango wa 12. Tulisoma hapa kwenye mlango wa 22. Hebu turudi kwenye mlango wa 12, lile agano alilofanyiwa Ibrahim. Sasa, agano hilo, kulikuwako na ninii tatu...maagano mawili.

<sup>38</sup> Sasa, Mungu anakamilika katika tatu. Tunazijua numerali za Mungu. Ukamilifu, katika tatu; ibada, katika saba; na kumi na mbili; na arobaini, ni majaribu; hamsini, ni Yubile; na kadhalika, Mungu katika—katika numerali Zake. Sasa, Mungu anakamilishwa katika tatu; kama vile Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu; na kadhalika.

<sup>39</sup> Sasa, kulikuwako na maagano mawili. Mojawapo lilikuwa ni agano la Adamu. Mungu alifanya agano na mwanadamu, "Kama ukifanya, Mimi nitafanya." Naye akalivunja. Ndipo Mungu akafanya agano na Nuhu; hilo lilikuwa ni agano la Nuhu, nalo likavunjwa.

<sup>40</sup> Sasa Yeye anafanya agano la Ibrahim. Na agano la Ibrahim, kulingana na Mwanzo mlango wa 12, lilitolewa bila masharti. Kwa hiyo ni la Milele, kwa sababu halina masharti. Si "Kama wewe ukifanya, Mimi nitafanya." Alisema, "Nimefanya!"

Nimelifanya tayari.” Si “*Nitalifanya.*” “Nimelifanya!” Hilo, loo, hilo, hilo linaiwekea imani msingi. Unaona, sio... Mungu ameyakinia kumwokoa mwanadamu. Akifanya agano, “Kama wewe ukifanya, Mimi Nami nitafanya,” angelilivunja. Lingine, “Utafanya, Nami nitafanya,” alilivunja. Mwanadamu hawezি kutimiza agano lake, kwa hiyo Mungu humwokoa mwanadamu kwa neema Yake, chini ya agano ambalo halina masharti, agano lisilo na masharti. Loo, jamani! Halina mwisho, hapakuwapo na lingine; tatu, kamilifu. Nuhu, Ibrahimu, na ninamaanisha... La. Adamu, Nuhu, na Ibrahimu. Sasa, hiyo ndiyo sababu sisi ni wana wa Ibrahimu, agano hilo haliwezi kwisha, kamwe halina mwisho, kwa maana halina masharti. Si... Si kwa sababu *wewe* unafanya jambo fulani; ni kwa sababu Mungu alifanya jambo fulani! Si kwa sababu ulimchagua Mungu; Mungu alikuchagua! Je! unaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.]

<sup>41</sup> Watu husema, “Loo, Ndugu Branham, nilimtafuta Mungu na kumtafuta Mungu!” Wala hukumtafuta! Ninachukia kukwambia hivyo, bali hukumtafuta. Mungu alikutafuta. Ilikuwa ni Mungu akikutafuta.

<sup>42</sup> Yesu alisema, “Hamkunichagua; Mimi niliwachagua. Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watanija Mimi.” Sasa, unaona, sivyo. Hakuna mtu anayeweza kujitokuza kwa chochote. Ni Mungu! Loo, ni ajabu sana vipi kuona ne—neema halisi ya Mungu, jinsi ilivyo!

<sup>43</sup> Na jinsi watu wameuchukua Ujumbe wa neema na kuufedhehi! Kama vile kanisa langu la thamani na ninyi watu wa thamani wa Kibaptisti, mnapoifedhehi neema namna hiyo, kweli mmeiweka kwenye mchafuko.

<sup>44</sup> Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, “Ndugu Branham, sasa unajua wewe ulikuwa Mbaptisti mzuri.”

Nikasema, “Ningali ninajisikia jinsi hiyo, bali nimepanda juu kidogo.”

<sup>45</sup> Akasema, “Vema, sasa angalia,” kasema, “Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kwamba ana haki. Ibrahimu angefanya nini zaidi ila kuamini?” Kisha akasema, “Tunapomwamini Mungu, tunampokea Roho Mtakatifu.”

<sup>46</sup> Nikasema, “Ni tofauti jinsi gani na Mtakatifu Paulo! Mtakatifu Paulo alisema, katika Matendo 19, ‘Je! mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?’ Si *wakati* mlipoamini; ‘tangu’ mlipoamini!”

<sup>47</sup> Akasema, “Vema, Ibrahimu alimwamini Mungu, hivyo tu ndivyo angaliweza kufanya.”

<sup>48</sup> Nikasema, “Kweli. Lakini basi Mungu alimpa agizo la tohara, kama uthibitisho ya kwamba Yeye alikuwa ameipokea imani yake.”

<sup>49</sup> Na endapo kamwe hajapata kukutahiri kwa Roho Mtakatifu, Yeye hajaipokea imani yako bado. Hiyo ni kweli. Hiyo ni tohara ya moyo na ya roho. Mungu anamtoa Roho Mtakatifu kama uthibitisho ameipokea imani yako. Sasa, kama ukiacha kuamini, na kuvurugavuruga mambo; na umwamini Mungu tu, Mungu atautahiri huo moyo. Na hilo hukatilia mbali kutokuamini kote, huukatilia mbali ulimwengu na kutokuamini kote kutoka kwako; ndipo basi unasimama, Neno peke yake. Yesu alisema, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu; basi ombeni lolote mtakalo, mtapewa.”

<sup>50</sup> Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi. Liko chini ya mhemuko, liko chini ya elimu, liko chini ya kanuni za imani. Si ajabu, limebanwa! Unaona? Kwa hiyo tunahitaji tohara, kukatilia mbali kitu hicho chote. Mrudieni Mungu na Neno Lake, na mliamini jinsi liliyvoandikwa pale, wala msibishane Nalo. Dumuni tu Nalo. Mungu alifanya ahadi, Mungu hutimiza ahadi Yake. Hawezi kufanya jambo lingine lolote ila kuitimiza ahadi Yake, na abaki Mungu.

<sup>51</sup> Sasa agano hili lisilo na masharti. Si “Kama utafanya, Mimi Nami nitafanya, bali nitafanya baadaye,” ama kitu kama hicho; “Tayari nimekupa nchi hiyo, pamoja na Uzao wako baada yako!” Amina. Unaona, amelifanya tayari! Ni kazi iliyomalizika.

<sup>52</sup> Ulisema, “Kwa Ibrahimu Yeye alifanya jambo hilo.” Naam, si kwa Ibrahimu tu, bali kwa Uzao wake baada yake.

<sup>53</sup> Na endapo sisi ni Uzao wa Ibrahimu, ni kazi iliyomalizika. “Wale aliotangulia kuwajua, Yeye aliwaita; wale aliowaita, aliwahesabia haki; wale alio wahesabia haki, Yeye tayari amewatukuza.” Unahofu nini? Hiyo ni kweli. “Naye mpinga Kristo, katika siku za mwisho,” kulingana na Ufunuo, “aliwadanganya wote walioishi juu ya uso wa nchi, ambao majina yao hayakuandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo” (tangu ule uamsho wa mwisho? La) “kabla ya kuwekwa misingi ya dunia.” Huo ndio wakati jina lako lilipoandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, wakati Mwana-Kondoo alipochinjwa. Mungu alinenya Neno; lilikuwa katika mawazo Yake, katika wazo Lake, Yeye alinenya Neno na kila kitu kikatukia kwenye wakati huo tu. Hii ni Mbegu ya Mungu tu ikipata umbo, hivyo tu, Maneno Yake yakishuka. Sasa, wakati Nuru ya Mungu inapomulika kwenye hiyo, upesi Mbegu hiyo huitambua, kwa sababu imezaliwa na Mungu. Ni Uzao wa Ibrahimu, uliojulikana kwa Mungu tangu awali. Hiyo ndiyo sababu Nuru humulika, ni kuishika hiyo Mbegu. Kama ikininii . . .

<sup>54</sup> Tumekuwa na uamsho. Yoeli alisema. Tunabishana sana juu ya mvua ya vuli, tulikuwa na madhehebu yaliyoitwa “mvua ya vuli,” mvua ya vuli, mvua ya masika, mvua ya ndani, mvua ya nje. Nilikuwa nikisoma hivi majuzi.

Je! mnajua *mvua ya masika* inamaanisha nini katika neno la Kiebrania? Siwezi kulikumbuka sasa hivi; sikuliandika, nimelisahau. Lakini *mvua ya masika*, ile mvua ya kwanza, inamaanisha “*mvua ya kufundisha*.” Mvua ya pili ni Roho anayekuja juu ya kile kimekwisha kufundishwa, na kuleta mazao. Ni kwa nini tulikuwa na uamsho kama huo? Pentekoste, Baptisti, miti mingine yote ilitoa chipukizi zao, kama vile Yesu alivyo sema ingekuwa. Nasi tumeangua kitu gani? Wabaptisti walisema walipata “milioni moja zaidi katika mwaka wa ’44.” Angalia Katoliki, jinsi walivyoongezeka. Yaangalie madhehebu yote. Waangalie Wapentekoste. Tulifanya nini? Tulipanda mbegu za kimadhehebu, tukavuna mavuno ya kimadhehebu. Mbona, kanisa linapaswa kuwa limeshika moto kwa ajili ya Mungu wakati huu, kama kungalikuwako na mbegu ya Neno iliyopandwa kule nyuma, na kungekuwako na ishara, maajabu, miujiza, nalo kanisa hilo lingekuwa limeshikamana, moyo mmoja, kwa umoja, na tukipiga hatua kuelekea Zayuni, kwa ajili ya Unyakuo. Hiyo ni kweli. Tulifanya nini? Tulikuwa na hotuba za kiakili badala ya Neno. Tulikuwa na hoja dhidi ya Neno, na chochote kile.

<sup>55</sup> Hatuna budi kurudi kwenye Neno. Inatubidi... Tutafanya hivyo! Mungu alisema, “Nitarudisha, asema Bwana, miaka yote iliyoliwa na parare na tunutu.” Utachanua wakati wa jioni. Kutatokea mtu akiwa na Ujumbe, atairudisha mioyo, ama imani ya watoto iirudie Imani ya baba. Yeye aliahidi jambo hilo katika Malaki 4, ya kwamba angefanya jambo hilo, kuirudisha tena.

<sup>56</sup> Sasa, huyo si Eliya aliyenerenwa habari zake katika Biblia; Yesu alisema katika Mathayo 11, “Kama mnaweza kulipokea, Yohana pale alikuwa ndiye Eliya aliye kuwa aje,” wa Malaki 3. “Tazama, ninamtuma mjumbe Wangu mbele za uso Wangu,” Malaki 3, mtapata jambo hilo.

<sup>57</sup> Lakini kumbukeni, Malaki 4, Ujumbe unakuja, “Ile Siku ya kuogofya ya Bwana itakuja na itaiteketeza dunia nzima, na wenyе haki watatembea juu ya majivu ya waovu.” Hilo halikutukia baada ya Yohana. La, kama huo ulikuwa ndio, basi Maandiko yamepoteza nguvu Zake, Yalisema jambo ambalo halikuwa kweli. Tuna miaka elfu mbili tangu wakati huo, ulimwengu haujateketeza tangu wakati huo, hata kidogo. Wala wenyе haki hawajatembea juu ya ma—majivu ya waovu. Bali tungali tunangojea kile kitu fulani ambacho kitahitaji Imani, na kuirudisha imani ya watoto irudi kwenye Mti wa asili wa kipentekoste ambao uliliwa na parare, parare wa Kirumi, madumadu. Madhehebu yao yote na kanuni zao za imani ziliula zikaumaliza. Mungu alisema, “Nitaurudisha tena, katika siku za mwisho.” Na utarudishwa! Mungu atamtuma Roho Mtakatifu hivi kwamba, juu ya Neno lililopandwa, ambaye atarudisha. Neno la Mungu ni Mbegu ambayo mpanzi alitoka akaenda kuipanda.

<sup>58</sup> Sasa, agano lilitolewa bila masharti! Sasa, Israeli, ule uzao wa kawaida ulilabadilisha hilo, na kulipoteza katika Kutoka 19, walipofanya lile jambo la kijinga kuiondoa neema, nao wakakubali torati mahali pake. Jinsi Israeli walivyofanya kosa la kijinga sana pale!

<sup>59</sup> Angalieni! Mungu, baada ya kufanya agano na Ibrahimu, neema ilikuwa tayari imemtoa nabii-mkombozi kwa ajili yao huko chini Misri, kulitekeleza neno la Ibrahimu. Mnakumbuka Musa, chini ya kile kichaka, Mungu alisema, "Nimesikia kilio cha watu Wangu, Nami ninakumbuka ahadi Yangu." Kabla hakujakuwako na torati yoyote, neema iliitoa. Neema ilikuwa imetoa dhabihu kwa ajili ya makosa yao, mwana-kondoo. Neema ilikuwa imetoa agano, tohara, ilikuwa tayari imetolewa, kabla ya torati. Neema ilikuwa imetoa Nguzo ya Moto kuwaongoza, wakimfuata nabii, hakikisho ya kwamba nabii huyu alikuwa amewaambia Kweli, ndilo Neno alilokuwa akinena habari zake. Walijua ya kwamba Mungu aliliahidi, na hii hapa Nguzo ya Moto ikilithibitisha. Ni hakikisho maradufu jinsi gani! Amina. Neema ilikuwa imetenda jambo hilo!

<sup>60</sup> Bali walitaka jambo fulani wangaliweza kufanya wao wenyewe, kuwa na kanuni zao na madhehebu yao wenyewe, na kadhalika, kuwafanya Mafarisayo, Masadukayo, na jambo fulani wangaliweza kufanya wao wenyewe.

<sup>61</sup> Mwanadamu daima anajaribu kujiokoa mwenyewe. Huwezi kufanya jambo hilo! Mungu amefanya hivyo tayari. Inakubidi tu kulikubali jambo hilo na kuliamini.

<sup>62</sup> Nguzo ya Moto kuwaongoza na kuwaelekeza, kuwaongoza Njiani. Mamlaka, neema ilikuwa imetoa Mamlaka fulani kumhukumu adui yao na kuwaweka huru. Mamlaka yalikuwa yametolewa tayari. Walivuka Bahari ya Shamu. Walikuwa wamempiga Farao. Walifanya mambo haya yote kwa neema. Na ndipo wakabadilisha neema kwa torati, bali hilo halikuwa na uhusiano wowote na Uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

<sup>63</sup> Uzao wa kifalme umejaribu kufanya jambo lile lile, kurudi chini ya namna fulani ya kanuni za imani badala ya kuchukua neema na Neno, na kuliamini. Wakarudi nyuma. Bali kutatokea Uzao wa kifalme; tutalifikia hilo baadaye kidogo, mbele kidogo.

<sup>64</sup> Hebu na turudi nyuma sasa katika Mwanzo 12. Mungu alimwita Ibrahimu kwa neema. Si kwa sababu yeye alikuwa ni mtu wa tofauti; alikuwa tu ni Ibrahimu, mtu wa kawaida tu. Sio kwa sababu alikuwa ni kuhani ama mtu mashuhuri; alikuwa ni mkulima tu. Alikuwa ameshuka akaja kutoka kwenye mji wa—wa ule Mnara wa Babeli, pamoja na baba yake, nao walikuwa wameenda Ukaldayo, Uru wa Ukaldayo. Na, kule, alikuwa ni mkulima, labda alilima mchana na kuzalisha chakula chake. Alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, Sara. Nao hawakuwa na watoto, na Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka sabini na

mitano Mungu alipomwita, na Sara alikuwa na umri wa miaka sitini na mitano.

<sup>65</sup> Basi Mungu akamwambia Ibrahimu wakati alipomwita, Akasema, “Nitakufanya baba wa mataifa,” na atampa mtoto mchanga kwa Sara. Sasa, ye ye ali kuwa ni tasa. Naye mke ali kuwa, vema, miaka sitini na mitano, ali kuwa amekoma hedhi miaka kumi ama kumi na mitano. Ali kuwa ameishi naye tangu alipokuwa na umri wa miaka kumi na sita ama kumi na minane, dada yake wa kambo. Na, wao, ali kuwa ni mume kwake miaka hii yote mpaka alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, naye ali kuwa na sitini na mitano, na ndipo Mungu akashuka na kusema, “Nitakupa mtoto, kupitia kwake.” Naye hakusita katika ahadi ya Mungu, bali alia min!

<sup>66</sup> Ungeweza kuwazia mzee, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mwanamke, sitini na mitano, wakishuka kwenda, wakitetemeka, kuelekea kwa daktari, na kusema, “Daktari, ninataka uiandae hospitali sasa. Huenda tukakupigia simu usiku wowote, kwa sababu, unajua, tutazaa mtoto”?

<sup>67</sup> Daktari huyo angesema, “Naam, ndio, bwana, wewe ni... A-ha, a-ha, a-ha!” Mara wakishika simu, anasema, “Yafaa umfuate, kuna kasoro.”

<sup>68</sup> Na kila mtu anaye amini ahadi za Mungu anaonekana, na ulimwengu, “mwenda wazimu.” Paulo alisema, “Kwa njia inayo itwa ‘uzushi’, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu.” *Uzushi* ni “wendu wazimu,” tunajua. Ni upumbavu kwa akili ya kawa idha. Imani ni wenda wazimu kwa kila mtu ila Mungu na ye ye aliye na imani. Hiyo ni kweli.

<sup>69</sup> Lakini Mungu alimwahidi Ibrahimu, na Ibrahimu aka amini hayo. Kamwe hakusema, “Mungu, itawezekanaje?” Alisema, “Vema, Mungu, nina amini jambo hilo.” Nami ninaweza kumwona akienda nyumbani, akisema, “Sara, hebu na tushuke twende na kujinunulia yadi kadhaa za nepi, na tununue pini, na tununue vijatu. Tutampata mtoto.” Loo, jamani!

<sup>70</sup> Siku thelathini za kwanza zikapita, ama siku ishirini na nane, “Unajisikiaje, kipenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Mungu abariki we, tutampata, haidhuru!”

“Unajuaje?”

“Mungu alisema hivyo!”

<sup>71</sup> Wengine wetu wanaweza kuombewa usiku mmoja, na kuketi mkutanoni ambapo Roho Mtakatifu anashuka; na kesho yake asubuhi, kama hatujapata afya, hatujapona, kabisa, “Ni—ningali ninaumwa na tumbo kidogo. Siwezi kusogezza mikono yangu tena.” Ati wewe, Uzao wa Ibrahimu, husiti kwa ahadi ya Mungu kwa kutoku amini?

<sup>72</sup> Kitu fulani kinazuka kanisani, ibilisi anaweza kuingia mionganoni mwa ku—kundi la watu wazuri na kuingia mle na kuanza kulicharaza kusanyiko hilo kila mahali, muda si muda unajua, wengine wanasesma, “A-ha, nitaachana na Kitu hiki cha kale, kwanza kabisa hakikuwa na lolote.” Ati Uzao wa Ibrahim? Jamani, jamani! Kasoro ndogo ya kwanza ibilisi anayoweza kukuonyesha, ndipo wewe, umeachana Nalo. Ilionyesha kwanza kabisa hukuliamini.

<sup>73</sup> Yesu alisema, “Ufalme ni kama mtu aliyechukua jarife, na akaenda baharini na kulitupa baharini. Wakati alipoingia, alikuwa na kila kitu.” Hiyo ni kweli.

<sup>74</sup> Hilo ndilo ninii—hilo ndilo uamsho unaloshika. Jarife lina kitu gani ndani? Una vyura, buibui, kasa, kamba wa maji baridi, nyoka, na samaki. Haikuchukua muda mrefu hata kasa aliposema, “Vema, mahali hapa hapanifai,” anarudi moja kwa moja matopeni. Maskini buibui wa majini akaangalia kila mahali, na kusema, “Wuui! siwezi kucheza karata hapa.” Kwa hiyo huyoo anaingia matopeni tena, kama nguruwe kwenye kugaagaa kwake matopeni na mbwa kwenye matapiko yake. Hiyo ni kweli. Ati basi Uzao wa Ibrahim? Loo, jamani! Fedheha jinsi gani!

Uzao wa Ibrahim huliamini Neno la Mungu!

<sup>75</sup> Unaketi huko nyuma na kusema, “Naam, Mungu abarikiwe, Mimi ni Mpentekoste!” Kisha mtu fulani anahubiri jambo fulani kwenye Neno, na Hilo hapo limeandikwa moja kwa moja. “Haleluya, siamini Hilo. La, bwana.” Ati Uzao wa Ibrahim? Hee!

<sup>76</sup> Sasa, kama ni upuuizi fulani, hakika, usiuamini. Lakini endapo ni Neno, Hilo ni Kweli! Hiyo ni kweli. Uzao wa Ibrahim hulishikilia hilo Neno wala si chochote kinginecho.

<sup>77</sup> Mwezi mwengine umepita. “Sara, kipenzi, unajisikiaje sasa? Unajua, siku zingine ishirini na nane zimepita, unajisikiaje?”

“Hakuna tofauti, mpenzi.”

<sup>78</sup> “Utukufu kwa Mungu! Ni mwujiza mkuu zaidi kwa miezi miwili kuliko vile ingekuwa kama ilitukia mwezi uliopita.”

Mwaka mmoja ukapita. “Je! niweke kando vijiatu hivi vidogo?”

<sup>79</sup> “La, bwana, wewe ziweke hapo. Tutampata mtoto huyo!”

“Unajua je utampata?”

“Mungu alisema hivyo! Hilo latosha.”

Baada ya miaka ishirini na mitano kupita. “Unajisikiaje, Sara?”

“Hakuna tofauti.”

<sup>80</sup> “Utukufu kwa Mungu! Ni muujiza wa miaka ishirini na mitano zaidi sasa!” Hakusita katika ahadi ya Mungu

kwa kutokuamini, bali alipata nguvu, akilishikilia Neno la Mungu; na kuviiita vitu hivyo ambavyo havikuwa, kana kwamba vilikuwako. Kwa nini? Mungu alisema hivyo! Loo, jamani!

<sup>81</sup> Uzao wa Ibrahimu siku hizi, mbona, wale tunaowaita Uzao wa Ibrahimu, ni dhaifu kuliko mchuzi ultiotengenezwa kwa kivuli cha kuku aliyekufa kwa njaa. Naam, bwana.

<sup>82</sup> Mungu anawataka Wakristo wajasiri ambaو hulichukua Neno la Mungu, waishi au wafe. Ni mamaoja. Amina, “Mungu alisema hivyo!” Huo ndio Uzao wa Ibrahimu, uliozaliwa kwa Roho na kwa Neno la Mungu. Hilo ndilo linalodumu.

<sup>83</sup> “Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitapita kamwe.” Jambo ndilo hilo. Kile Mungu alichoahidi, Mungu anaweza kufanya. Mungu hashindwi. Hawezi kushindwa. Kuna jambo moja ambalo Mungu hawezi kufanya, na hilo ni kushindwa. Hawezi kushindwa, hilo ndilo jambo pekee asiloweza kufanya. Bali hawezi kushindwa. Wakati Mungu alipoliahidi, ni Kweli. Linadumu milele. Limekamilika milele. Mungu anaponena Neno, limetimia tayari.

<sup>84</sup> Dunia hii iliumbwba kwa Neno la Mungu tu. Yeye alisema tu, “Na iwe,” na ikawa. Amina. Vumbi lenyewe unalokalia usiku wa leo, ubao wenyewe unaokalia, si kitu ila ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Haleluya!

<sup>85</sup> Ninajisikia wa kiroho ninapowazia juu ya Ibrahimu, nikijua ya kwamba tunaweza kuwa Uzao wake, Uzao wa Ibrahimu pamoja na ahadi hizi zote. Si kulihakikisha tu, Mungu aliuinua mkono Wake, akaapa kwa nafsi Yake, ya kwamba angeitimiza. Kiapo, daima, agano huthibitishwa kwa kiapo, na Mungu aliapa kwa nafsi Yake maana hakuna aliye juu zaidi wa kuapia. Aliapa kwa nafsi Yake, ya kwamba angelilitimiza hilo.

<sup>86</sup> Sasa ni kitu gani ulimwengu, vipi, tuna—tuna shida gani sisi? Ahadi kama hiyo! Imani iliyojengwa kwenye kitu kama hicho, imani iliyojengwa! Neno lililoahidi mambo haya katika siku za mwisho, na hapa tunayaona yakutikia moja kwa moja mbele zetu, na bado tunakwepa wakati wote. Ati Uzao wa Ibrahimu? Loo, jamani! Ninawatakeni mshikilie jambo hilo, “Uzao wa Ibrahimu.”

<sup>87</sup> Mwanzo 12, kile Mungu alichohitaji kwa Ibrahimu kilikuwa ni utengano mkamilifu.

<sup>88</sup> Sasa, siku hizi, wanataka mtu wa watu. “Loo, tunapomchagua mchungaji, hana budi kuwa na nywele za kipilipili, na awe anatokea moja kwa moja huko Hollywood, unajua, na anaweza kusema “ah-mina” vizuri sana, na kuvala nguo zilizo nadhifu sana, na kuendesha kadilaki la hali ya juu sana, na—na kadhalika namna hiyo, naye ni mtu wa watu. Anafanya jambo hili. Naye atakunywa kinywaji kidogo mara kwa mara pamoja nasi, apate kuwa mtu wa watu. Yeye anahudhuria karamu za mabibi wazee, nao wanafuma na

kushona, na kushona na kufuma, na kuzungumza juu ya Bibi *Nanii*, na kadhalika, unajua, na yote namna hiyo. Nao inawabidi kuwa wa—wajichanganyao wa aina hiyo.”

<sup>89</sup> Mungu alisema, “Nitengeeni Paulo na Barnaba! Amina. Utengano! “Ondokeni kati yao wala msishiriki mambo yao machafu!” Mungu anataka utengano, kuangamizwa kabisa kwa dhambi. Kujitenga! Hiyo ndiyo shida ya siku hizi, sababu ya sisi kutoweza kuwa Uzao wa Ibrahim, hatuvezi kujitenga na mafundisho ya sharti pamoja na kanuni za imani, na kadhalika, yanayoitwa Ukristo, tuliedee Neno lililo hai. Jitengeni na kutokuamini kwenu, na mkaliamini Neno la Mungu. Mungu atalidhahirisha kwenu. Kweli.

<sup>90</sup> Mwanzo 12, Mungu alisema, “Jitenge na jamii yako yote na kila kitu kinachokuzungu.” Loo, jamani, hatuvezi kujitenga na kucheza karata! A-ha!

<sup>91</sup> Nilienda kwenye mgahawa fulani leo, wakati ndugu alipoingia pale. Nilimwangalia tineja mhuni akiingia pale. Nami na mke wangu tulikuwa tukijaribu kula, ndipo nikawazia, “Mungu asifiwe! Hebu tuharakishe, mpenzi, kabla mtu fulani hajaingia.” Ndipo tineja mmoja akaingia pale, akienda kifichifichi. Ningegopa kukutana na kijana huyo penye giza. Ndipo akaweka si—sindano ya mashine pale ndani na, ama santuri, na kuanza kucheza ule upuuzi wa bugi-wugi, naye amesimama pale, akienda namna *hii*, unajua, akijipigapiga namna *hiyo*. Nikasema, “Masalaale, rehema!”

<sup>92</sup> Meda akasema, “Usi—usiende pale kulipa bili hiyo. Wewe ngojea papa hapa, hebu niende pamoja nawe.” Alihofu.

<sup>93</sup> Mtu yejote katika hilo, mambo tulio nayo siku hizi, taifa la Kikristo, loo, ni kitu cha namna gani! Utengano! Asilimia tisini ya hao wanaimba kwenye kwaya, akina Elvis Presley, na Pat Boone, na wote hao, na Peabody Ernie, chochote wanachomwita kule chini. Mbona, ni wabaya kuliko Yuda Iskariote! Yuda Iskariote aliuza, na akapata vipande thelathini vyta fedha; Elvis amemshinda, alipata milolongo kadhaa ya makadilaki na kupendwa sana na watu. Na kwa sababu watoto hawa wadogo wanaona upuuzi huo wote, wanasema, “Yeye ni wa kidini sana.” Huyo ni ibilisi! Kweli kabisa! Mungu havumilii upuuzi kama huo. Hicho ni cha kupofusha hapa katika siku za mwisho.

<sup>94</sup> Rudini kwenye Neno, “Jitengeni na mambo yote maovu, wala msiguse kitu chao. Nitawapokea.”

<sup>95</sup> Injili, tunapaswa kuishika kwa mikono mitupu! Si kwa glavu za kanisa, kumpigapiga mtu mgongoni, ambalo husababisha kiota kilichojaa mayai yaliyooza tena, kumfanya mtu fulani mtu wa wilaya, ama mzee wa kanisa, askofu, ama kitu kama hicho. Ni kitu gani kinachoninii... Mnawezaje kuwa na imani wakati mnajiheshimu, mnaheshimiana ninyi kwa ninyi? Tunamtazamia Mungu, na Yeye peke yake! Heshima hutoka kwa Mungu.

Yeye Ndiye wa kuheshimiwa. Tunamheshimu kwa kushikilia Neno Lake kama tochi, na kuenenda kama mwanamume ama mwanamke mbele za Mungu. Hakika. Utengano mkamilifu!

Mwanzo 13, Lutu alirudi nyuma. Kumbukeni. Wana ninii kidogo...

<sup>96</sup> Baada ya kujitenga, na kuvuka mto na kuingia nchini, Mungu alisema, “Ibrahimu, nitakupa yote sasa, bali hujanitii kikamilifu.”

<sup>97</sup> Na muda si muda mwajua, kulitokea ugomvi mdogo kuhusu wachungaji, na mionganoni mwa wachungaji wa ng’ombe wao, na Mwanzo 13 (ni jambo gani lililotukia?), wale wachungaji wa Lutu na wachungaji wa-wa Ibrahimu. Mwangalie Ibrahimu, lile tendo la kindugu, yeje alisema, “Hebu na kusiwe na ubishi kati yetu. Sisi ni ndugu.” Lutu aliwakilisha kanisa vuguvugu. Naye akasema, “Āngalia, jichagulie. Chochote utakacho, nenda ukakichukue. Ukienda mashariki, nitaenda magharibi, kadhalika. Ama, ukienda magharibi, nitaenda mashariki. Ukienda kaskazini, nitaenda kusini, na kadhalika. Wewe jichagulie.” Naye Lutu tayari alikuwa ameenda Misri na alikuwa akikutupia jicho kupendwa kidogo na watu, alikuwa na fedha kidogo mfukoni mwake.

<sup>98</sup> Hapo ndipo kanisa lilipofanya kosa lake. Ninasema hili kwa uchaji, ndugu. Kanisa la Kipentekoste lingekuwa ni bora zaidi likiwa na tari, huko nje pemberi, likiwa na wanaume na wanawake wa mtindo wa kale, likiwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuliko wangalikuwa katika madhababu hizi kubwa na nyumba za maiti wanamoishi siku hizi chini ya upuuzi huu wote mtupu na takataka. Hiyo ni kweli. Wanataka kufanya kama hao wengine. Hapo ndipo tulipolipata. Kwa nini hamkukaa jinsi mlivyokuwa, jinsi Mungu alivyanza nanyi? Kitu kile kile mllichobishania, nanyi mligueka na kufanya jambo lile lile.

<sup>99</sup> Hivyo ndivyo Lutu alivyofanya, akashuka kwenda Misri na, muda si muda mwajua, akaikazia Misri macho yake. Kisha akaangalia huko akauona Sodoma, anasa, starehe. Ndipo akaenda mashariki kuelekea... Kumbukeni, akaenda mashariki badala ya kwenda magharibi pamoja na Ibrahimu. Alielekeea mashariki kwa sababu ilikuwa ndiyo njia ya anasa. Alielekeea upande wa mashariki.

<sup>100</sup> Hivyo ndivyo kanisa limefanya siku hizi, unaona, walirudi nyuma. Kama nilivyosema jana usiku, jua huchomoza mashariki na linaenda magharibi. Naye Mwana wa Mungu alizuru Mashariki kwanza, na ameelekea magharibi. Wameizima kabisa, katika miaka elfu mbili. “Lakini itakuwako nuru wakati wa jioni,” nabii huyu alisema. Badala ya kumfuata Mwana, wanarudi nyuma mahali ambapo Mwana alikuwa. Siku hizi ikitokea kwamba useme jambo juu ya uponyaji wa Kiungu, kuhusu unabii, kuhusu karama tisa za kiroho, ama kitu

fulani; "Hebu na turudi nyuma tuone kile Moody alichosema, kile Sankey alichosema, kile Knox alichosema, kile Calvin alichosema." Wao waliishi katika siku ambayo Mwana alikuwa akiangaza nuru kule; sisi tunapiga hatua kuelekea kwenye ukamilifu! Amina!

<sup>101</sup> Mwanasayansi Mfaransa alisema, yapata miaka mia tatu iliyopita, akalithibitisha kwa kufingirisha mpira kuizunguka dunia, alisema, "Kama mtu ye yote angepata kwenda kwa mwendo wa kasi mno wa maili thelathini kwa saa, nguvu za uvutano zingewaondoa duniani." Akalithibitisha kisayansi. Je! unafikiri sayansi hurejea hilo? La, bwana! Wanazo zinazoenda kwa karibu maili elfu mbili kwa saa, wakijaribu kuzifanya ziende mbio zaidi. Hawaangalii nyuma kwenye hilo.

<sup>102</sup> Lakini wahudumu, "Tutarejea nyuma tuone yale Moody aliyosema, yale Sankey aliyosema." Huko ndiko Mwana *alikokuwa*. Hapa ndipo alipo siku hizi! Liko kwenye Pwani ya Magharibi, katika wakati wa jioni, haleluya, likitoa Nuru za jioni! Sio kurudi nyuma kwenye kuhesabiwa haki kwa Luther ama kutakaswa kwa Wesley; bali tuko kwenye siku ya mwisho, amina, wakati Nuru za jioni zinapoangaza, wakati tukiwa kwenye wakati wa mwisho. Mfuaneti Mwana.

<sup>103</sup> Lakini Lutu alirudi nyuma kwa sababu ilikuwa ni rahisi, anasa. Hebu mwangalieni Bibi Lutu wakati alipofika huko nyuma. Mbona, hapana shaka alikuwa ni malkia wa mashirika ya jiji hilo. Lutu akawa ndiye meya. Loo, ndugu, walifanikiwa, mbona, ninamaanisha kusema!

<sup>104</sup> Hivyo ndivyo watu wamemchukua Bibi Lutu siku hizi. Angalieni jinsi watu wetu wanavyofanya siku hizi. Angalieni watu wetu makanisani, angalieni tu jambo hilo. Waangalieni wanawake wetu, waangalieni siku hizi.

<sup>105</sup> Ni—nilikuwa Hollywood hivi...ama Los Angeles, hiyi majuzi, nilikuwa nikimngoea Ndugu Arganbrite aje. Na pale alisimama msichana, akaja pale. Nikaangalia, na nikaduwaa. Nikamwangalia. Nikawaza, "Mimi ni mmishenari. Nimeona tauni, nimeona ukoma, bali sijapata kuona kitu kama hicho." Alikuwa na mmoja wa ile mitindo ya kukata nywele kichwamaji, hizi, unajua, unajua, unazoita, zilionekana kama kichwamaji, mwajua, Ma—Mama wa Taifa, naam, kama Yezebeli, namna hiyo. Naye alikuwa na bluu na kijanikibichi; na huenda alikuwa ni mwanamke mrembo; lakini upuuzi huo wote alio nao, alionekana kama Mhotentoti wa Afrika. Nikaenda pale, nilikuwa nikienda kumwombea mwanamke huyo. Nikawaza, "Mama, samahani, mimi huwaombea wagonjwa. Sijapata kuona kitu chochote kama hicho. Hebu niambie ni kitu gani." Ndipo mwanamke mwingine akaanza kuzungumza naye, naye alikuwa vile vile. Loo, jamani!

Loo, unasema, “Huyo alikuwa ni Mpresbiteri.” Mpentekoste! Hakika.

<sup>106</sup> Na Biblia ilisema, “Ni aibu kwa mwanamke kukata nywele zake.” Akizikata, anakiaibisha kichwa chake. Anamwaibisha malaika, malaika wa Nuru. Wale malaika Saba wa Kanisa, wale wanaoileta hiyo Nuru watadumu na Neno. Mwenye kufedhehesha! Anapaswa kuwa na nywele kichwani mwake. Jamani, kitu kama hicho! Na ilikuwa ni makosa kwao kufanya hivyo. Katika—katika Upentekoste wa kwanza, ilikuwa ni makosa. Ni kitu gani kilitendeka? Mlipiga mbio vema, ilikuwaje?

<sup>107</sup> Na baadhi ya wanawake wetu wa Kipentekoste mnavaa hizo nguo zinazoonekana kama mnyama aliyechunwa ngozi, hapa nje mahali fulani wakijaribu... Hiyo ni kweli! Sisemi jambo hilo kwa utani. Hapa si mahali pa kufanya mzaha. Hii ni mimbara.

<sup>108</sup> Mwanamke fulani aliniambia usiku mmoja. Niliwaambia jinsi walivyokuwa wakivaa nguo. Kasema, yeye akasema, “Mimi sivai kaptura. Ni—ni—ninavaa suruali ndefu.”

<sup>109</sup> Nikasema, “Hiyo ni mbaya zaidi. Mungu alisema, ‘Mwanamke atakayevaa vazi linalompasa mwanamume, ni chukizo mbele za Mungu.’” Kweli!

<sup>110</sup> Na hebu nikwambie jambo fulani, mama, wewe, msichana, unayevaa huko nje, utawajibika kwenye siku ya hukumu kwa kufanya uzinzi.

Unasema, “Mimi ni safi tu kama yungiyungi.”

<sup>111</sup> Naam, bali Yesu alisema, “Mtu atakayemwangalia mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Huenda isikubidi kufanya tendo hilo. “Mtu atakayemchukia ndugu yake bila sababu, amekwisha kumwua.” Unaona, wewe ufanye jambo moja tu. Na kama huyo mwenye dhambi akikuangalia jinsi ulivyovaa, umejipamba jinsi ulivyo, umerejea nyuma, na kusukumwa nje, na kusukumwa ndani, na umevaa nguo kama hizo, kisha unatoka nje. Sasa hebu sikiliza, huo si utani! Hii ni Injili! Nawe unajipamba hivyo, na mwenye dhambi fulani akuangalie na kukutamani. Kwenye siku ya hukumu, wakati anapojobu kwa kufanya uzinzi, ni nani aliyesababisha jambo hilo? Ulilisababisha. Utawajibika kwake kwa kuwa ulijianika namna hiyo.

<sup>112</sup> Mbona, unasema, “Wao—wao hawashoni nguo za aina nyingine.” Wanatengeneza cherehani, na wangali wanauzu vitambaa. Hakuna udhuru hata kidogo! Ni kwa sababu mmeliacha Neno! Hilo halipendwi na watu. Hilo ni gumu.

<sup>113</sup> Mhubiri mashuhuri alikuja hivi majuzi, akaniwekea mikono, kasema, “Nitakuwekea mikono yangu na kumtoa pepo huyo.”

Nikasema, “Nini?”

<sup>114</sup> “Kuzungumza juu ya hao wanawake jinsi hiyo.” Kasema, “Watu wanakuona kama nabii.”

Nami nikasema, nikasema, "Mimi si nabii yeyote."

<sup>115</sup> Akasema, "Wanakuchukua kuwa hivyo, Ndugu Branham." Kisha kasema, "Unapaswa kuwa ukiwafundisha hao watu, hao wanawake, jinsi ya kupata baraka kuu za kiroho. Na unaendelea kuwaambia juu ya wao kukata nywele zao na vitu kama hivyo. Hawatasikiliza hayo."

Nikasema, "Ninajua hivyo."

Kasema, "Mbona usiwafundishe mambo makubwa zaidi?"

<sup>116</sup> Nikasema, "Ninawezaje kuhubiri, kuwafundisha aljebra wakati hata hawajui ABC zao, si hata adabu ya kawaida?"

<sup>117</sup> Na wewe mwanamume mtakaowaachilia wanawake wenu wafanye hivyo, nina heshima duni sana kwenu kuwa wanaume wa Kikristo, Uzao wa Ibrahim. Amina! Afadhali niliache hilo, nitawafanya ninyi nyote mwamke na kwenda nyumbani. Vema. Moja ya siku hizi mtakosa kupata kitu fulani Huko juu.

<sup>118</sup> Unasema, "Haileti tofauti yoyote." Ilileta kwa Paulo. Ilileta kwa Mungu, katika bustani ya Edeni. Biblia ilisema ya kwamba mwanamke anapaswa kuwa na nywele ndefu! Na bila ya hizo, uko wapi? Vema, unasema, "Haileti tofauti yoyote." Biblia ilisema inaleta! Usimruhusi ibilisi kuhojiana nawe, na kukwambia, "Ni jambo la kisasa, ni sawa." Si sawa! Ulisema, "Sikujua hivyo hapo awali." Unaajua jambo hilo sasa. Unaona? Lichunguze na uone kama ni kweli. Nitaliacha hilo, unaona. Vema.

<sup>119</sup> Mwanzo 13, mamboleo, a—ha; rudi mahali Mwana alipokuwa, sio Mahali alipo Mwana; mahali Mwana alipokuwa, haidhuru. Mke, nawazia, mke wa Lutu, jinsi alivyoingia katika jamii!

<sup>120</sup> Hivyo ndivyo tulivyointia katika jamii. Hivyo ndivyo sisi Wapentekoste tulivyointia mle. Tulifanyika, tulijiundia dhehebu dogo *hapa*, na moja dogo dhidi yake, moja dhidi ya lingine, na dhidi ya *hili*, nao wanafanya... Mliingiza kitu chochote. Hiyo ni kweli kabisa.

<sup>121</sup> Samwel aliisema nini wakati Israeli walipotaka—walipotaka kuwa na mfalme, walipomtaka Sauli awe mfalme? Samwel aliwajia, na kusema, "Je! nimewahi kuchukua pesa zenu nipay riziki? Je! nimewahi kuwaambia lolote katika Jina la Bwana ila lililotimia?"

<sup>122</sup> Loo, wao wakasema, "Hakika, wewe ni nabii wa Mungu. Ulitwambia Kweli, na uliyosema yalitimia, bali tunataka mfalme, kwa vyoyote vile."

<sup>123</sup> Na popote mlipoanza kuachilia mambo, na kuachilia *hili* na *lile*, na kitu kingine chochote kikaingia jinsi hiyo, mlififanya wa kisasa. Nalo kanisa ni kama tu hao wengine siku hizi. Tunachohitaji ni kufagiliwa nyumba kwa Kipentekoste! Hiyo ni kweli kabisa. Amina. Ni aibu kwamba inambidi Mbaptisti

kuwaambia jambo hilo, sivyo? Bali ni Kweli. Kweli! Ninaiamini Biblia, ninaamini Neno la Mungu ni kweli. Vema.

<sup>124</sup> Ibrahimu, ndipo Ibrahimu akachukua ninii...katika kifungu cha 14 cha mlango wa 13, baada ya Lutu kujitenga, naye Ibrahimu akamwamini Mungu kabisa, basi Mungu alipomjia. Sasa Yeye yuko tayari kumbariki.

<sup>125</sup> Na mpaka kanisa la Kipentekoste litakapoacha kanuni zake zote za Imani na mafundisho ya sharti, na kutenda kama ulimwengu na kuonekana kama ulimwengu, na kuzungumza kama ulimwengu, na kukaa nyumbani Jumatano usiku kuangalia *Tunampenda Susie* badala ya kuhudhuria mkutano wa maombi, na vitu kama hivyo, kumtolea zaka zako mhubiri fulani hapa nje anayeendesha namna fulani ya kipindi cha redio kudhahiki kitu kile hasa unachotetea, hiyo ni kweli, na upuuzi wote wa namna hiyo ambao unaendelezwa katika jina la pentekoste, ni fedheha!

<sup>126</sup> Mimi huwahubiria Wafanya Biashara Wakristo, baina ya mataifa. Wapo wengi wao wanaoketi hapa sasa. Hapa hivi majuzi usiku, hapa karibu mwaka mmoja uliopita, imekuwa, nilikuwa huko Jamaica. Nao walikuwa na watu wote mashuhuri wa kisiwa hicho huko usiku mmoja, nao hawa watu wakisimama, wakishuhudia, “Utukufu kwa Mungu! Nilikuwa mfanya biashara duni huko pembeni. Haleluya, Nina kadilaki nne sasa. Utukufu kwa Mungu!”

<sup>127</sup> Ndipo nikarudi huko kwenye Moteli ya Flamingo usiku huo, nikasimama pale, nikasema, “Ninawaonea aibu!” Nikasema, “Ninyi watu hapa kumwakilisha Kristo, mkijaribu kumwambia mfanya biashara kwamba una kiasi gani cha mali, ye ye ana zaidi ya uliyo nayo ama utakayowahi kupata.” Hiyo ni tofauti kubwa sana na wale wapentekoste wa mwanzoni. Wapentekoste wa mwanzoni waliuza waliyokuwa nayo, na kuwagawia maskini, kisha wakaenda na kuihubiri Injili. Kweli!

<sup>128</sup> Maskini mwimbaji mmoja wa Kiswidi kutoka Chicago, sitalitaja jina lake. Yeye ni ndugu yangu wa thamani. Alisimama, akasema, “Ndugu Branham, ingawa wewe... Tunaamini kwamba wewe ni nabii, bali nitakwambia sasa hivi, ‘Uko makosani.’”

Nikasema, “Niambie ni wapi, ndugu.”

<sup>129</sup> Akasema, “Vema, hao watu waliuza waliyokuwa nayo, na kuyaweka kwenye miguu ya wale mitume, nao wakayagawa.” Akasema, “Lilikuwa ni tendo baya sana walilowahi kufanya.”

<sup>130</sup> Nikasema, “Unamaanisha kuniambia Roho Mtakatifu anatenda tendo baya?”

Akasema, “Lilikuwa ni kosa. Nitakuthibitishia.”

Nikasema, “Kwa nini?”

<sup>131</sup> Kasema, "Basi wakati mateso yalipoibuka, hawakuwa na mahali pa kwenda. Walitanga-tanga, kila mahali."

<sup>132</sup> "Sawa kabisa katika mapenzi ya Mungu, wakihubiri Injili kokote walikoenda. Hawakuwa na mahali pa kurejea." Mungu hafanyi makosa. Kweli! Loo, ni tofauti jinsi gani; pentekoste iliyokuwapo, na Pentekoste iliyopo. Naam, hilo hapo.

<sup>133</sup> Baada ya Ibrahimu kujitenga na Lutu, jinsi hasa Mungu alivyomwambia afanye. "Jitengeni na kila dhambi ituzingayo kwa upesi, ondooleeni mbali kila kitu!" Hapo, ndipo Mungu akasema, "Ibrahimu, sasa wewe ni mrithi wa mambo yote. Angalia mashariki, angalia magharibi, angalia kaskazini, angalia kusini, tembea nchini kote, yote ni yako!" Amina.

<sup>134</sup> Unatenga kitu chako, wewe mwenyewe na dhambi, kutokuamini. Kuna dhambi moja tu, na hiyo ni kutokuamini. Kufanya uzinzi siyo dhambi, kunywa pombe siyo dhambi, kusema uongo siyo dhambi; hayo ni matokeo ya kutokuamini. Kama uliamini, usingeyafanya mambo hayo. Hakika. Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:24, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele," hiyo Zoe, Roho Mtakatifu, kwa sababu aliamini. Vyema. Sasa, mpaka utakapompokea Huyo, wewe ni mwaminio wa kujifanya, ambaye uko kwenye kundi hilo. Lakini wanapoamini kabisa, wakijitenga, ndipo basi unapojitenga na kutokuamini kwako kote, na kumwamini Mungu, unatembea kikamilifu, ukizitimiza zile Amri, ukifanya kila tendo jema, ndipo Mungu atasema, "Kila ahadi katika Kitabu hicho ni yako." Amina. "Yote ni yako! Achana na Hayo, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, yote ni yako!" Amina. "Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu likae ndani yenu, mwaweza kuomba mtakalo, litatendeka." Kitu gani? Huna budi kujitenga, kwanza, na kutokuamini kwako.

Unasema, "Ndugu Branham, unaifanya ngumu mno."

<sup>135</sup> Yesu alisema, "Katika siku za Nuhu kulikuwako na wanane waliookolewa. Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu."

<sup>136</sup> "Ni wangapi hao, Ndugu Branham?" Huenda wakawa ni elfu nane, labda milioni nane, sijui ni wangapi. Bali watakuwa katika uchache. Mmoja kutoka kwa kila mia moja elfu, ama kitu kama hicho, ningesema. Vema.

<sup>137</sup> Imani ya akilini, imani ya kichwani, bila tukio la kuzaliwa mara ya pili, mhemuko, kanuni za imani ya kikanisa! Kama Roho Mtakatifu wa kweli na halisi yumo mile ndani, ataliitikia hilo Neno; nalo hilo Neno litaishi kama vile hasa alivyosema litaishi, kwa sababu Roho yuyo huyo aliyelinena ndiye anayelinena kuititia kwako. Halina budi kuishi. Hakika, linaishi. Si wewe unayesema, bali ni Baba anayeishi ndani yako, Yeye Ndiye anayenena. Vema.

Ibrahimu, mrithi wa vitu vyote.

<sup>138</sup> Mimi, nilipojazwa na Roho Mtakatifu kama vile ninyi watu mlivyojazwa, nilitaka nitembee kupitia, na, kama kwenye njia tao kubwa yenyе maduka, kila kitu humo ni mali yangu. Mimi ni mrithi wa kila sehemu yake. Na kama nilirithi njia tao iliyoja maduka, ni—ningependa kujuwa nilicho nacho. Nilipokuwa Mkristo, nilitaka kujuwa kipi ni mali yangu. Kwa hiyo kama nilikuwa na njia tao iliyoja maduka, ningeipitia, na kuvuta mtoto wa meza na kuona kilicho hapa ndani, na kuangalia *huku* na kuona kilicho mle ndani; kitu fulani kinaonekana kuwa juu kidogo pale, ninachukua ngazi ya kupandia na kupanda nikakifikia. Ningechunguza kwamba ni kitu gani. Kitu fulani kinaonekana kidogo siwezi kukifikia hapa, ningepiga magoti yangu na kuanza kuomba mpaka nikifikie. Ni mali yangu! Mungu alikiahidi. Uponyaji wa Kiungu, Nguvu za Mungu, miujiza hii yote na ishara na maajabu, Yeye aliahidi.

<sup>139</sup> Unasema, “Ndugu Branham, mambo haya yanatendekaje?” Kwa ahadi ya Mungu. Amina.

<sup>140</sup> Uzao wa Ibrahim! Utukufu! Ninajisikia vizuri. Ninaweza kuonekana mwenda wazimu na kutenda kama mwenda wazimu, bali niachenii. Ninajisikia vizuri zaidi hivi kuliko nilivyojisikia kwingine. Unaona?

<sup>141</sup> Mlango wa 14, tunamwendea Ibrahim, sasa tunaona katika mlango wa 14 kile kilichotukia. Wale wafalme walishuka kutoka sehemu mbalimbali za nchi, nao walikuwa wameungana na wafalme wa Sodoma, nao wakaingia na kuuteka Sodoma, wakamchukua Lutu; ndugu ya Ibrahim katika Bwana, wakamchukua mateka, ndugu yake vuguvugu wa kimadhehebu, nao wakaondoka naye. Sasa, kumbukeni, Mungu ndiyo kwanza amwambie Ibrahim ya kwamba kila kitu katika hiyo nchi kilikuwa ni mali yake.

<sup>142</sup> “Na wenye upole watairithi nchi.” Ati mnasema sisi ni wenda wazimu? Tutaichukua nchi, yale yaliyo juu ya nchi! Hakika, sisi ni warithi wake.

<sup>143</sup> Hebu mwangalie Shetani, alimwambia Yesu, “Kama utaanguka na kunisujidua, nitakupa ulimwengu huu.” Falme zote zinatawaliwa na ibilisi, kila moja ya hizo. Yesu alisema hivyo. Biblia inazungumzia jambo hilo. Kila taifa na kila ufalme unatawaliwa na ibilisi. Na Shetani alisema, “Haya ni mali yangu. Haya ni yangu. Nitakupa Wewe kama utanisujidua.”

<sup>144</sup> Yesu alijua atayarithi katika ule Utawala wa Miaka Elfu, kwa hiyo akasema, “Rudi nyuma Yangu, Shetani.” Yeye alijua atayarithi.

<sup>145</sup> Na leo hii wanazungumza juu ya wenda wazimu wanaomwabudu Bwana na kuzaliwa mara ya pili. Wanaogopa huko “kuzaliwa mara ya pili.” Kabisa hawalitaki wazo hilo, nao walikubadilisha na kitu kingine. Moja la hayo limekubadilisha na kupeana mkono; hilo lingine, nyunyizo dogo la maji; hilo

lingine, kutoa ulimi wake na kula kipande kidogo cha mkate; hilo lingine, kucheza-cheza sakafuni. Ni Kuzaliwa! Kama nilivyosema hivi majuzi usiku, "Kuzaliwa ni mchafuko, sijali kuko wapi. Kama kuko kwenye kizimba cha nguruwe ama chumba cha hospitalini, ni kuzaliwa, ni mchafuko." Na vivyo hivyo Kuzaliwa upya, kunakurarua-rarua, lakini kutokana na mchafuko huo unakuja Uhai mpya. Amina. Naam.

<sup>146</sup> Ibrahimu alijua ya kwamba kila kitu kilikuwa ni mali yake, kwa hiyo basi wakati Lutu alipoingia, alisema, "Sasa ngoja kidogo." Lutu alitekwa na mikono mikatili ya adui. Akasema, "Huyo ni ndugu yangu, nami nitamfuatilia." Sasa kumbukeni, kulikuwako na kama wafalme saba au wanane pale waliokuwa wameungana, nao wakashuka wakaenda na kutwaa kila kitu na kutoroka nacho. Nao walipotoka, Ibrahimu aliwachukua watumishi wake na kumfuatilia, apate kumrejesha ndugu yake aliyepotea. Huyo ni Mkristo halisi, alimfuatilia ndugu yake aliyepotea. Je! alifanya nini wakati alipompata? Aliwapiga hao wafalme; kisha akarudi, akimleta ndugu yake, baada ya vita.

<sup>147</sup> Angalieni, kulikuwako na Mfalme mmoja aliyekuja kumlaki, wakati akirudi, Melkizedeki. Melkizedeki, Yeye alikuwa ni nani? Hakuwa na baba, hakuwa na mama. Kamwe hakuzaliwa, kamwe Yeye hafi. Hana baba, hana mama, hana mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa maisha Yake. (Hakuwa Mwana wa Mungu; kwa sababu yeye alikuwa na Baba na mama, wote walizaliwa na wakafa, na kufufuka tena.) Bali mtu huyu kamwe hakuwa na baba wala mama, Yeye ni Mungu! Hakika, Ndicho Kitu cha pekee kilicho cha Milele.

<sup>148</sup> Naye alikutana na Ibrahimu baada ya vita kwisha, akiuonyesha Uzao wa Ibrahimu; baada ya sisi kwenda kumtafuta ndugu yetu aliyeanguka, na vita vimekwisha. Melkizedeki alimwandalia nini? Divai na mkate, ushirika. Amina. Wakati vita vimekwisha, ndugu! Kurudi, akimrudisha nyumbani tena ndugu yake aliyepotea, akimrejesha. Na wakati vita vilipokwisha, Melkizedeki alimplaki na kumpa ushirika. Yesu alisema, "Sitakula wala kunywa tena kabisa uzao wa mzabibu hata siku ile nitakapounywa mpya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu." Naam, bwana. Sasa vita vilikuwa vimekwisha, Ibrahimu alikuwa amerudi, mlango wa 14; ndipo yule Mshindi akamlaki, hapo alipokuwa akija pamoja na yule Mshindi.

<sup>149</sup> Mwanzo 15 sasa, kabla hatujafunga, maana ni wakati wa kufunga sasa. Sikilizeni jambo moja zaidi kabla hatujaondoka.

<sup>150</sup> Nami itanilazimu kuendelea na jambo hili kesho usiku tena, maana kabisa sijalifikia somo langu, sijapafifikia mahali pangubado, juu ya Yehova-Yire. Ninataka kulifikia kule chini, Bwana akipenda.

<sup>151</sup> Sasa kwenye mlango wa 15, nimepata hapa kuwa agano lilithibitishwa kwa Ibrahimu, kule kuhakikishwa kwa lile agano.

Kwa maneno mengine, ni wakati Mungu alipokula kiapo, na wakati Mungu alipotoa ahadi na kumhakikishia Ibrahimu ahadi hiyo. Katika mlango wa 15, tunaona jambo hilo, kule kuthibitishwa kwa kiapo ambacho Mungu alisema.

<sup>152</sup> Ibrahimu alimwambia Mungu, “Mrithi wa nyumba yangu bado ni huyu Eliezeri wa Dameski.”

<sup>153</sup> Naye akamwambia, “Ila huyo siye mrithi wako, kwa maana mrithi wako ni yule atakayetoka kwenye tumbo lako mwenyewe.” Naye akamwahidi.

Kasema, “Nitajuaje jambo hili?”

<sup>154</sup> Loo, sasa, ndugu, hiki hapa kitu kitakachowaamsha! Mwangalieni. Yeye alisema, “Nenda kaniletee mbuzi wa kike mwenye umri wa miaka mitatu, mtamba wa kike, mwenye umri wa miaka mitatu, na kondoo dume mwenye umri wa miaka mitatu.” Ndipo Ibrahimu akawachukua, na hua wawili... hua na njiwa.

<sup>155</sup> Sasa, hua na njiwa wana uwakilisho; hawa wanyama wenye umri wa miaka mitatu, na walikuwa ni watatu. Sasa Yeye anaenda kufanya hilo agano, kuthibitisha agano hilo. Sasa sikilizeni kwa makini, msilikose. Na kisha tutalichukua kesho usiku wakati atakapokutana naye hapa tena, Bwana akipenda. Angalieni.

<sup>156</sup> Sasa Yeye alisema, “Nichukulie m—mtamba mwenye umri wa miaka mitatu, mbuzi jike mwenye umri wa miaka mitatu, na kondoo dume mwenye umri wa miaka mitatu, njiwa, na hua.”

<sup>157</sup> Ndipo Ibrahimu akaondoka akaenda akawachukua hao wanyama, naye akawapasua vipande viwili na kuwaweka, kipande kwa kipande; bali hua na njiwa, hakuwapasua hua na njiwa. Hua na njiwa ni wa familia moja. Kwa hiyo hao waliwakilisha uponyaji wa Kiungu, ambao katika maagano yote mawili ni kwa imani, unaona, ambapo wanaponywa; mmoja tu kwa mwingine, huyo mwingine. Kama lile agano la kale ilikuwa na uponyaji wa Kiungu ndani yake, ni zaidi sana vipi Hili lilivyo nao! Unaona, kama ile dhabihu ya kale ilikuwa na uponyaji, vipi kuhusu Hii ambayo ni bora zaidi! Unaona?

<sup>158</sup> Sasa, bali angalia kile alichofanya hapa. Yeye aliwachukua hawa wanyama watatu na kuwapasua vipande, na kuwaweka, kipande kwa kipande. Ndipo Ibrahimu akarudi. Sasa, hiyo ilikuwa ni dhabihu. Naye akawalinda hata juu lilipokuwa likitua. Na ndege wakashuka kutoka hewani, wakaja juu ya dhabihu ya Ibrahimu, wala mizoga. Na Ibrahimu akawawinga mbali, akawafukuza.

<sup>159</sup> Huu ni mfano wa kitu gani? Uzao wa Ibrahimu katika siku za mwisho, wakiwafukuza pepo kutoka kwenye Dhabihu, wakiwafukuza kutoka kwenye Dhabihu. Mungu aliiyahidi, ile Dhabihu, Kristo, yeye yule jana, leo, hata milele, na hao

wote pepo wasioamini wakijaribu kuila. Mtu wa Mungu, Uzao wa Ibrahimu, anasimama pale akiwatoa pepo, mbali Nay! Kuthibitisha agano sasa, lile thibitisho, likionyesha ya kwamba Uzao wa Ibrahimu katika . . . ninamaanisha Uzao mwaminifu wa kifalme. Kumbukeni, ule uzao wa maumbile ya kawaida ulishindwa, kwa maana ulikubali torati badala ya Neno la neema. Na vivyo hivyo umeshindwa katika huku “kushindwa kabisa”, katika Mataifa katika siku ya mwisho. Bali kuna Uzao, Uzao wa kifalme ukiwa na Neno, ni mwaminifu, ukiwatoa pepo, ukifanya ishara kubwa na maajabu, ukiondoa kutokuamini kote kutoka kwenye Neno, ukidumisha usafi wa Dhabihu, ukidumisha utakatifu wa Neno, ukidumisha heshima Yake; bila kuweka chochote Kwalo, kuongeza chochote Kwalo; kulitunza, ukililinda, kuzuia lisiguswe na chochote.

<sup>160</sup> Sasa angalia, usingizi mzito ulimjia Ibrahimu, mauti. Na baada ya huo usingizi mzito, aliona tanuru la moto, ambalo ni kuzimu, likitoa moshi, ambamo kila mwenye dhambi anapaswa kwenda. Lakini hapo mbele Nuru nyeupe ilipita. Iangalie hiyo Nuru ndogo nyeupe, ilienda katikati na kuzitenganisha dhabihu hizi, ikaenda katikati yake, Mungu akithibitisha yale Yeye atakayofanya kupitia kwa Uzao wa Ibrahimu.

<sup>161</sup> Sasa, Wayahudi daima waliamini ya kwamba Mungu alikuwa ni Mmoja. Naye Mungu ni Mmoja. Lakini alikuwa akionyesha hapa, kwa dhabihu hizi tatu safi, ya kwamba utatu wa Mungu utawakilishwa katika Mmoja katika Uungu kwa jinsi ya mwili.

<sup>162</sup> Sasa angalieni katika siku za-zamani za kale, katika siku za kimashariki, wakati agano lilipofanywa, hivi ndivyo walivyolifanya. Kama vile, tulikuja na tukamchinja mnyama, tukampasua mnyama huyo vipande viwili, kisha tukasimama katikati ya mnyama huyo, na hapo tukaliandika agano. Sasa huko Uchina . . .

<sup>163</sup> Jinsi ambavyo huko Japani, wanapofanya agano, wanachukua chumvi kidogo nao wanasisimama na kufanya ahadi zao, nao wanarushiana chumvi. Hivyo ndivyo ilivyo huko Japani, wanavyofanya agano, wanarushiana chumvi. Chumvi ni ladha, unaona. Nao wanarushiana chumvi, hilo ni—hilo ni a—agano.

<sup>164</sup> Sasa hapa Marekani, jinsi tunavyofanya agano, tunatoka tunaenda kula chakula, na kupeana mikono, “Nipe mkono wako, jamani. Hilo limekubalika?” “Limekubalika!” Hilo ni agano.

<sup>165</sup> Lakini zamani za kale, katika wakati wa Ibrahimu, jinsi walivyofanya agano ilikuwa ni kuchinja dhabihu, na kusimama katikati ya hiyo dhabihu; halafu basi, walipofanya hivyo, waliandika agano hilo kwenye ngozi ya mwana-kondoo huyo, kisha wakaipasua. [Ndugu Branham anararua kipande cha karatasi, na kutoa mfano—Mh.] Mmoja akachukua kipande kimoja, na huyo mwingine hicho kingine. Sasa wakati agano hili

lilipothibitishwa na kuletwa pamoja, hakuna mtu angaliweza kuliiga hilo. Unaona, halina budi kuumana, herufi kwa herufi, jinsi tu liliwyokuwa hasa. Hilo linaonyesha ya kwamba mwenyewe halisi wa kipande hiki alikuwa na sehemu, hili ni agano lile lile, kwamba havina budi kuja pamoja na kuumana kikamilifu.

<sup>166</sup> Na Mungu hapo alikuwa akimwonyesha Ibrahimu, ya kwamba kupitia kwa Uzao wake, Mungu Mwenyewe atafanyika mwili na imbidi kutenganishwa pale Kalvari; ambapo Kristo, akiwa ni Mungu duniani, Yeye alitenganishwa. Mungu alimpasua, Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, na akautoa Uhai Kwake; kisha akaufufua huo Mwili, apate kuketi kwenye Kiti Chake cha Enzi Mbinguni; halafu akairudisha Roho Yake juu ya Kanisa, ili kwamba Kanisa lipate kuwa na Roho yeye—yeye yule aliyekuwa katika Kristo kulifanya liungane, ikimfanya Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele! Kuthibitishwa kwa agano, Mungu akilithibitisha agano. Mungu akitenganisha, akiuraru Uhai kutoka kwa Kristo, Mwanawе, akiitoa Roho ndani Yake; kama vile alivyowapasua wanyama hawa vipande viwili, akisimama katikati ya hao wanyama. Ile Nuru, Mungu Mwenyewe, ilienda katikati yao, akionyesha kwamba Yeye aliutenganisha ule Mwili: ule Uzao, Uzao wa kifalme; kisha akaichukua hiyo Roho na kuirudisha juu ya Kanisa. Nalo Kanisa la siku hizi linaloenda kumlaki Kristo, itabidi liwe na Roho yeye yule aliyekuwa naye, maana itabidi iwe ni Herufi kwa Herufi, Neno kwa Neno. Naye ni Neno! Yesu alisema, “Yeye” (kiwakilishi nafsi) “aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.” Kuthibitishwa kwa agano, Úzima ulio ndani ya Kristo utakuwa ndani ya Kanisa, ule Uzao wa kifalme wa Ibrahimu.

<sup>167</sup> Hebu kidogo, ndugu, juu ya Pentekoste. Walipokuwa katika chumba cha juu...Kama ulipata kuwa kule na kuuona ule mchoro halisi, jinsi ulivyochorwa, walizunguka kwa kipandio upande wa nje wakaingia kwenye chumba cha juu. Walikuwa na mishumaa midogo ya mafuta ya mizeituni ikiwaka. Walikuwa kule juu kwa muda wa siku kumi usiku na mchana, huku milango yote imefungwa. “Na mara ukaja uvumi kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. Ndimi za moto, ndimi za moto zilizotengana, zilimkalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, wakatoka mbio wakaingia uwanjani, wakinena kwa lugha zingine.”

<sup>168</sup> Angalia, huo Moto uliotengana ulikuwa ni nini? Ulikuwa ni ile Nguzo ya Moto, Roho Mtakatifu, Mungu, Malaika aliyewaongoza kupitia nyikani, Yule ambaye alidihirishwa mbele zao. Mungu alikuwa amejitenganisha na kijigawanya Mwenyewe mionganoni mwa watu hao, Roho Mtakatifu, na pamoja sisi ni Kanisa la Mungu aliye hai. Agano! “Ibrahimu na Uzao

wake baada yake, Uzao wa kifalme.” Uhai ule ule uliokuwamo ndani ya Kristo, umo ndani ya Kanisa, ukifanya kazi zile zile ambazo Kristo alifanya. Amina. Ni jambo zuri jinsi gani, enyi marafiki!

<sup>169</sup> Wakati umekwisha sasa hivi, sina budi kufunga huu. Naam, nitachelewa mno. Nitaninii . . . Je! inaweza kuwa ni sawa kama nikianzia papa hapa kesho usiku? Ninataka sana kuufikia *Yehova-Yire*. Lakini ninawatakeni mwone ni kitu gani, kwamba lile jambo la kukiri kuwa Mkristo, ndugu, wakati umewadnia ambapo kanisa halina budi kuninii . . . Kama Mungu alifanya ahadi hizi, ni za kweli. Hazina budi kutimia.

<sup>170</sup> Hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. Hili linakera na ni gumu. Linakatakata. Sipendi kufanya hivyo. Mhudumu huyu aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, kwa nini *nini*, unafanya hivyo?”

<sup>171</sup> Nikasema, “Sina vipindi vyta televisheni vyta kudhaminiwa, redio. Ninaenda tu jinsi hii, ambapo ninaweza kwenda popote.” Nikasema, “Ni nani atakayewaambia? Inapaswa kuwepo na sauti mahali fulani itakayolisema.”

<sup>172</sup> Sasa Mungu yupo hapa, enyi marafiki. Na kama umejiita mwenyewe Uzao wa Ibrahimu, na unafikiri ya kwamba wewe . . . Sasa usininii . . . Sikilizeni, ni nafsi yako, ewe rafiki. Ni nafsi yako. Usibahatishe nayo, maana usiku wa leo huenda ukawa ndio mara ya mwisho unapopata nafasi kwa hiyo. Kama unayaonea aibu maisha yako, ukijiita mtoto wa Mungu, na ukiishi jinsi ambavyo umeishi; nawe unaamini ya kwamba Neno la Mungu ni kweli, nawe umekosea, ninakutaka uombe kwa muda kidogo tu, umwombe Mungu ayachunguze maisha yako. [Ndugu Branham anatalia—Mh.] Ombeni tu.

<sup>173</sup> Baba wa Mbinguni, huenda huu ukawa ndio usiku wa mwisho kwa wengi wetu. Tunafikiria, siku chache zilizopita usiku huko Los Angeles, mama mzee mwenye umri wa miaka sabini akiketi pale, naye akaenda madhabahuni na kuyatoya maisha yake kwa Kristo. Usiku huo akafa kitandani. Neema ya Mungu, saa hiyo ya mwisho. Baada ya kuishi miaka hiyo yote pasipo kumjua Yeye, ndipo akamwita katika saa hiyo ya mwisho. Neema ya ajabu.

<sup>174</sup> Baba Mungu, nena na mioyo hapa usiku wa leo. Unajua kusudi la jambo hili. Unajua, Baba, hapana—hapana budi uje wakati ambapo jambo fulani halina budi kufanya. Tu-tunaona hali ya mambo, na jinsi inavyozidi kuwa mbaya wakati wote. Nasi tunatambua ya kwamba wakati wa kanisa la Kipentekoste, katika siku za mwisho, ndio Wakati wa Kanisa la Laodikia, ule wa pekee ambapo Kristo alitolewa nje ya kanisa, amesimama, akibisha akijaribu kurudi ndani. Ee Mungu, uturehemu.

<sup>175</sup> Na kama vile nilivyowakemea dada zetu usiku wa leo, Bwana, jalia wajue ya kwamba huko nyuma mwanzoni, lilipoanza na, ilikuwa ni Hawa. Na ndilo hili hapa tena. Injili huja kwa Neno, na jinsi ambavyo yeye alifanya kile alichofanya (na hebu angalia siku hizi) kwa kuhoji; mwangalie mama yake, kile alichowazia kilikuwa ni tofauti, Biblia ile ile.

<sup>176</sup> Mungu, ndugu zetu, kwa vile ilinibidi kuwakemea, Bwana. Mimi nina ari, na—na—nawapenda. Unajua ninawapenda, Bwana. Mimi—mimi—mimi nimejitolea miaka thelathini na moja hapa kwa ajili yao, Nawe umelithibitisha Neno Lako, na chochote kile. Bwana, sijui nifanye nini jingine. Lakini ninapoliona kanisa ambalo ninalipenda, kanisa la Kipentekoste, lile lililosimama nyuma yangu na kuniunga mkono; Mungu, upendo wa Kikristo ndio unaokufanya Wewe uliondolee uovu. Upendo ndio unaokufanya Wewe kutenda hilo, Baba. Unajua ndio. Nami ninajaribu kuwaambia watu hawa, “Msijaribu kwenda huko nje, mkifanya mambo haya.” Ngu—nguzo zimeshushwa, nasi tumeanguliwa kupitia kwa kanuni zetu mbalimbali za imani na mambo ambayo tumeyaingiza kanisani, na kuondoka kwenye zile siku za miujiza, tunaenda mbali na uponyaji wa Kiungu, tukaachana na ji—jinsi watu wanavyopaswa kutenda na kuvaa.

<sup>177</sup> Nawe ulifanya agano na Adamu, na lingine na Hawa; uliweka maagano mbalimbali, na tofauti kabisa, na ukasema ni kosa kwa mwanamke kutenda kama mwanamume. Anapaswa awe wa kike. Anapaswa kuwa wa kike wala si wa kiume. Na siku hizi anajaribu kuwa wa kiume; naye mwanamume, wa kike.

<sup>178</sup> Bwana, na—nalo hili papa hapa kwenye siku za mwisho, papa hapa kwenye Pwani ya Magharibi, papa hapa mwishoni mwa ustaarabu, tunaona wanawake wakifanya upotovu ule ule hasa kama walivyofanya mara ya kwanza. Nao huu hapa, umeingia mionganii mwa dada zetu, Ee Mungu, hilo ndilo linalouvunja tu moyo wangu, Bwana. Nami najua kama linanifanya mimi (mwenye dhambi) kujisikia namna hiyo, linakufanya nini Wewe, kuona jinsi amekuwa mungu mke. Na madoido haya ya ajabu-ajabu ya Hollywood ya dhambi! Na ilikuwa ni jambo ovu kwao kwenda kuona sinema, ndipo ibilisi akawarushia moja kwa moja nyumbani mwao, na—na kila namna ya vipindi visivyokaguliwa, na upujufu mtaani.

<sup>179</sup> Na, Ee Mungu, ni—ni wakati wa wenda wazimu. Ni wakati wa kurukwa na akili. Ni—ni wakati ambapo mtu hatatulia na asikilize, na kuchunguza. Na chini ya mihemuko, na kadhalika, wao wangali wanadai kuwa Uzao wa Ibrahimu. Mungu, jinsi ambavyo ulisema ingekuwa, roho hizo zingefanana sana katika siku za mwisho, pamoja na maigizo, hata karibu ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini. Nayo ndiyo hii hapa. Mungu, usiache watu hawa, usimwache mmoja afanye hivyo. Nakusihi,

Baba. Ninawaombea, kila mmoja. Katika Jina la Bwana Yesu, tujalie.

<sup>180</sup> Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu. Ningewafanyia jambo lolote. Na kama nikiwakemea tu watu kusudi niwe mgomvi, Mungu kamwe asingekuwa pamoja nami; sistahili kuwa hapa, ninapaswa kuwa huko mahali fulani nikipasua kumi ama kitu kama hicho. Lakini, enyi marafiki, hiyo—hiyo ni kweli, lichunguzeni na mwone kama siyo Maandiko. Nayo yanapaswa kufunuliwa katika siku hizi za mwisho.

<sup>181</sup> Sasa je! wewe ni mwaminifu vya kutosha? Wewe kweli, chini ya hilo ganda la nje, je! kuna kitu fulani halisi kukuhusu, ambapo uko tayari kukubali kwamba umekosea? Wakati kila kichwa kikiinamishwa, kila moyo, na kujiweka wakfu kindani kwa uchaji, ungeweza kuinua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham. Niko makosani. Kwa neema ya Mungu nitajiweka sawa”? Mungu akubariki, wewe, wewe, wewe. Hiyo ni kweli, inua mkono wako, Yeye anauona. Kwenye roshani, Mungu anawaona. Inueni mikono yenu. Je! ninyi—ninyi . . . Haya basi.

<sup>182</sup> Sasa *hapa* pana baadhi yenu wanawake mmeketi hapa mkiwa na nywele fupi, wala hamjauinua mkono wenu. Mna shida gani? Mko makosani! Kamwe msijaribu kumlaki Mungu namna hiyo. Mtahukumiwa hakika tu kama ninavyosimama kwenye mimbara hii. Mnataka kuniambia kanisa la Kipentekoste limefikia hali hiyo hata li—li—limekuwa baridi sana hata linajionea aibu kukubali ya kwamba limekosea? Msifanyo hivyo. Mungu na awarehemu.

<sup>183</sup> Ninaamini. Nina imani. Hebu ningojee tena. Mungu akubariki hapo, mpenzi. Mungu akubariki, dada. Hilo ni zuri. Inueni . . . Hilo . . . Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Huenda ukalikubali sasa; asubuhi huenda ikawa ni kucheleta sana, saa moja kutoka sasa huenda ikawa ni kucheleta sana. Mungu akubariki. Huo ni uaminifu. Mungu akubariki. Sema, “Nimekosea.” Inahitaji mtu mnyofu kukubali wamekosea. Hicho ni kitu fulani halisi. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Naam. Naam, endeleeni tu kuomba. Mungu akubariki. Kama nikikosa kuuona mkono wako, Yeye hakosi. Anajua kila wazo lililo moyoni mwako. Hiyo ni kweli kabisa. Mungu akubariki, ninauona mkono wako. Hilo ni zuri. Mungu akubariki, ewe msichana. Mungu akubariki, dada. Hilo ni zuri.

<sup>184</sup> Mungu akubariki hapo, ewe msichana. Naam, badiliko la barabara za maisha. Kabla mambo haya hayajaukausha moyo wako mbichi, mgeukie Mungu sasa, mpenzi. Hiyo ni kweli, fanya hivyo. Nina binti mdogo pale wa karibu rika lako. Mungu akubariki, mpenzi. Mungu akubariki. Naam, Mungu akubariki, dada.

<sup>185</sup> Na wewe je, ndugu? Jionee aibu, kumwacha mke wako afanye hivyo na kuvaat kaptura, na kuvaat namna hiyo na kwenda mtaani. Ati unajita mwana wa Mungu? Hivi huoni haya? Mungu akubariki. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Hilo ni sawa, kubali umekosea. Naam. Kama ukininii . . .

<sup>186</sup> Yeye anayezificha dhambi zake hatafanikiwa; yeye azitubuye dhambi zake atapata rehema.” Mungu akubariki. Kuna wengine? Huko nyuma kwenye roshani, huko juu kwenye roshani. Yeye anakuona huko juu. Anajua kila wazo lililo moyoni mwako.

Sasa inueni vichwa vyenu kwa dakika moja.

<sup>187</sup> Nasema kuna karibu hamsini ama sitini humu chumbani walioinua mikono yao, vijana kwa wazee. Asanteni. Hao ni mabibi na mabwana halisi. Ninawathamini. Kuna—kuna matumaini kwenu mnapokuwa radhi kukubali ya kwamba mmekosea.

<sup>188</sup> Kabla sijatoa wito wa madhabahuni, nitaziombea leso hizi.

<sup>189</sup> Baba wa Mbinguni, leso hizi zinawakilisha watu wagonjwa, mama na baba wanaongojea, watoto. Wakati mmoja, tunafundishwa katika Biblia, ya kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo vitambaa na leso. Watu waliomwona, walijua ya kwamba Roho wa Mungu alikuwa juu yake. Paulo alikumbuka ya kwamba Elisha alimwambia yule mwanamke Mshunami, aliyemwambia Gehazi, “Ichukue fimbo hii uende ukaiweke juu ya mtoto huyo.” Alijua ya kwamba kile alichogusa kilibarikiwa. Paulo, walichukua kutoka mwilini mwake vitambaa na leso, na pepo wachafu wakawatoka watu, magonjwa yakatoweza. Sasa, Bwana, sisi si Mtakatifu Paulo, bali Wewe ungali ni Mungu, Mungu yeye yule.

<sup>190</sup> Siku moja Israeli walikuwa njiani wakiwa moja kwa moja kwenye wajibu wao, wakielekea kwenye nchi ya ahadi. Na kitu fulani kikawatenganisha na nchi ya ahadi, Bahari ya Shamu. Mwandishi mmoja alisema, “Mungu alichungulia kupitia kwenye hiyo Nguzo ya Moto, kwa macho yenye hasira, ndipo bahari ikaogopa, ndipo ikafingirisha kuta zake na kuifungua njia kavu kwa ajili ya Israeli wapate kuvuka waingie kweye nchi ya ahadi.”

<sup>191</sup> Mungu, leso hizi zitakapopelekewa wagonjwa na wanaoteseka, jalia Mungu wa Mbinguni achungulie kupitia Damu ya Mwanawe Mwenyewe, jalia ibilisi, anayewashikilia hao wagonjwa, aogope na kuondoka wakati leso hizi za tunu za mukutano huu usiku wa leo, ambapo Neno na Kweli zimetimizwa; wagonjwa na wanaoteseka wapate afya; miyo ambayo imevunjika, na inayoshuka kwenda katika Nyumba ya Mfinyanzi katika dakika chache; jalia ya kwamba ibilisi ataondoka, nao watu watavuka waingie kwenye nchi hiyo ya

afya njema waliyoahidiwa na Mungu. Ninazituma leso hizi, Katika Jina la Yesu Kristo, kwa kusudi hilo. Amina.

<sup>192</sup> Na Mungu anaujua moyo wako. Anaijua hali yako. Kuonyesha tu; na hebu niwaambie, kuna kundi kubwa la watu humu ndani ambaao hawakuinua mkono wao, ambaao walipaswa kuuinua. Sasa, kama nikikuita moja kwa moja kutoka humu jukwaani, niseme wewe u nani, itamuudhi mtu fulani. Sasa, mmeniona nikifanya hivyo mara nyngi. Nilipata kujuu, Yesu alisema, "Acheni magugu na ngano vikue pamoja. Malaika watakuja na kuyafunga magugu na kuyachoma moto kwanza."

<sup>193</sup> Na sasa ni wakati wa kufunga. Kila mmoja wao anaingia kwenye muungano wa makanisa, madhehebu yote. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Muungano wa Ulimwengu, Baraza la Makanisa, kila dhehebu linavutwa kuingizwa ndani yake, ndilo jambo kubwa linaloendelea. Wote wakirudi Roma kama tu walivyoahidi, "alamu iliyofanyiwa mnyama," mamlaka, muungano wa makanisa, jinsi hasa Mungu alivyosema ingetimia. Hayo hapo, wakikuachilia, na kukwambia ya kwamba ni sawa kufanya *hivi*, na wanaogopa kusema jambo lolote juu yake, wakihofu itakatiza posho mahali fulani.

<sup>194</sup> Hebu niwaambie jambo fulani, ndugu yangu, dada, Mungu na awafunulie ya kwamba ninawapenda. Si niwe tofauti, ni kuwa mwaminifu. Kamwe usibahatishe hata kidogo. Usingelevuka taa nyekundu, kwa ajili ya mwili wako. Na nafsi yako je! Usivuke moja ya taa nyekundu za Mungu.

<sup>195</sup> Baadhi yenu ni wagonjwa. Amini kwa moyo wako wote. Mtu ambaye ana hamu kubwa ya kitu fulani, kuwa tu na imani. Nitawaonyesha kama kweli Yeye, kama ni Kweli ama sivyo. Ibrahimu, mnakumbuka yule Malaika alimjia Naye akafanya nini? Angalieni kama ni jambo lile lile.

<sup>196</sup> Huyu hapa maskini mwanamke mmoja ameketi hapa, papa hapa, ana kansa. Ana uvimbe, naye anangojea upasuaji. Ananiangalia sasa, na hizo shanga nyekundu shingoni mwake. Umetoka Portland. Lakini kama utaninii... Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hiyo ni kweli. Unaona? Sikujuu, sisi hatufahamiani. Bali hiyo ni kweli. Sasa unawezajaze kuketii hapo, ukiwa na imani ya kutosha kugusa vazi la Kristo wakati huyo Malaika wa Nuru anapokuja juu yako namna hiyo, neema ya Mungu? Ikubali, mama. Iamini. Si hivyo tu, bali iamini Injili yote.

<sup>197</sup> Huyu hapa mwanamke fulani ameketi papa hapa nyuma. Angalia hapa, mama. Unaugua ugonjwa wa utumbo mpana. Amini kwa moyo wako wote. Naam, sikujuu mimi. Amini kwa moyo wako wote, na upate afya.

<sup>198</sup> Yupo mwanamume anayeketi karibu na wewe, hana budi kwenda nyumbani. Hawezi kukaa zaidi. Ana shida ya masikio yake. Ana shida ya... Amekuwa na mafua, na

ikasababisha kukohoa. Hawezi kupona, ni—ni namna fulani ya—ya matatizo mengi yaliyomkumba. Hiyo ni kweli, bwana. Unafanya kazi kwenye namna fulani ya kiwanda cha vitu kama makombora ama kitu kama hicho. Inakubidi kurudi kazini kwako. Hatufahamiani. Endapo mambo hayo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Iwapo una imani ya kutosha kumgusa Bwana Yesu, kwa nini usiwe mwanamume halisi na uliamini kwa moyo wako wote?

<sup>199</sup> Yupo mama anayeketi huko nyuma, yeye ana namna fulani ya ugonjwa wa ngozi mikononi mwake. Hata hajui ni kitu gani. Daktari hata hajui ni kitu gani. Amekuwa nao kwa miaka na miaka. Loo, ataukosa, kweli kabisa. Bibi Daniels, McDaniels. Haya basi. Ida McDaniels, amini kwa moyo wako wote. Simjui mwanamke huyo, sijapata kumwona. Bali kuna Nuru juu yake.

<sup>200</sup> Ni kitu gani? Yeye anakuju! Naye anajua ya kwamba umekosea! Mungu yeye yule anayenena kuitia kwangu jinsi hii, ananena kuitia kwangu kwa Neno.

<sup>201</sup> Sasa, kila mtu humu ndani anayetambua Uwepo wa Mungu, na unajua ya kwamba umekuwa makosani, hebu na tuje madhabahuni sasa. Njoni hapa kwa dakika moja, hebu niwaombee. Kama unajua umekuwa makosani, unataka kuyatubia makosa hayo. Unataka kuwa Mkristo halisi tangu sasa na kuendelea, njoo hapa madhabahuni. Sitaki kulitaja jina lako, i—isingekuwa ni tabia ya Kikristo. Huko juu kwenye roshani, shukeni chini, hii ndiyo nafasi yenu. Shukeni chini sasa! Njoni madhabahuni, mseme, “Ninakuja, Bwana.” Mwenye dhambi, njoo madhabahuni, hii huenda ikawa ndiyo nafasi yako ya mwisho. Hivi huwezi kuja wakati sisi...kinanda kinapiga vizuri sana, “Ninakuja, Bwana, ninakuja sasa Kwako.” Vema, kila mtu na aimbe sasa.

Ninakuja, Bwana!  
Ninakuja sasa Kwako!

<sup>202</sup> Hivi huwezi kuja? Shukeni mje kutoka kwenye roshani, shukeni chini. Njoni huku juu. Nanyi je! ninyi watu mnaodai kuwa ni Wakristo, Uzao wa Ibrahim? Mungu awabariki, wanawake. Mungu awabariki, dada zangu. Naam. Mungu hakika ataliheshimu. Ninyi ni waaminifu. Labda mchungaji wenu ameshindwa kuwaambia jambo hilo. Nenda nyumbani ukachukue Biblia yako, uone kama ni kweli, ama si kweli. Mnajua ni kweli, kabla hata sijasema jambo lolote. Ninyi wanawake wa Kipentekoste, msingejipodoa bure. Hakuna kitu katika Biblia juu ya vipodozi; ila tu Yezebeli, aliupodoa uso wake na kadhalika, kwa rangi na takataka. Lakini kuko katika Biblia kuhusu ninyi kuwa na nywele ndefu, “Ni jambo lisilo la kawaida kwa mwanamke hata kuomba akiwa amekata nywele zake, kunyoa nywele.”

...kwako!

<sup>203</sup> Je! unataka kujiweka sawa na Mungu, Uweponi wakati Yeye akiwa hapa? Njoo huku! Simama, mtetee! Simama kwa miguu yako ushuke uje, useme, “Ninakuja. Nita—nitashuhudia. Ninataka ulimwengu mzima ujue ya kwamba nimekosea, nami ninataka kuwa sawa mbele za Mungu.” Njoo sasa!

Ninakuja, Bwana!  
 Ninakuja sasa Kwako!  
 Nioshe, nisafishe katika Damu  
 Iliyotiririka kutoka Kalvari.

Tena, kila mtu!

Ninakuja . . .

Njoni. Wapo wengine huko, kumbukeni. Naam, hiyo ni kweli.

. . . mimi, nisafishe katika Damu Yako  
 Iliyotiririka kutoka Kalvari.

<sup>204</sup> Wapo watu wangali wanakuja, endeleeni tu kuomba. Sasa, enyi marafiki, mimi sipendi sana kushawishi. Ninaamini Neno hufanya kazi Yake linapotoka kuja huko mliko. Msimhuzunishe Roho Mtakatifu. Huenda ikawa ndiyo nafasi ya mwisho utakayopata kuwa nayo; natumaini siyo. Unajua vile inavyofanya kukuona wewe wakati unapokubali umekosea? Inaniambia ya kwamba kuna kitu fulani halisi pale, ya kwamba kweli unataka kutenda haki. Sasa kwa kinanda tu, polepole ukiweza, ninapozungumza. Njoni, enyi watu, njoni moja kwa moja. Ninawatakeni mwendelee kuja. Mnajua kile watu hawa wamefanya? Wengi wa hawa ni wafuasi waanzilishi wa kanisa, nao wanajua nimesema Kweli.

<sup>205</sup> Si *mimi*. Ni kama tu wakati Musa aliposhuka akaenda kule kuwaambia watu juu ya Bwana; Naye Bwana, chini ya ile Nguzo ya Moto, akathibitisha Neno na kuonyesha ya kwamba lilikuwa ni kweli. Nguzo hiyo ya Moto ipo papa hapa pamoja nasi. Ni Kristo yeye yule, akifanya jambo lile lile kwa ajili ya wakati wa Mataifa, kama alivyoahidi kufanya.

<sup>206</sup> Inanifanya niamini nini? Ya kwamba wewe ni mwaminifu moyoni mwako. Ni kitu gani kilichokufanya usimame kwa miguu yako? Ni kwa sababu kitu Fulani kilikuwa kimekuzunguka, ambacho kilisema, “Umekosea.” Sasa huyo alikuwa ni Mungu, kwa maana baadhi yenu mnaona aibu kusimama hapa namna hiyo mbele za watu, baada ya kutubu. Lakini inaonyesha ya kwamba kitu Hiki halisi kilichosema, “Umekosea,” na kilikuja kwa Neno, kwa utambuzi. Kupitia . . .

<sup>207</sup> Karama hizi zinatumwa kanisani kwa sababu gani? Karama ya kwanza ni ipi? Jambo la kwanza ni lipi? Mitume (ambao ni wamishenari), manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti. Zote kwa jumla ni kwa ajili ya kulikamilisha Kanisa.

<sup>208</sup> Na ni wapi Neno la Bwana linakuja, kwa nani? Neno la Bwana lilimjia nabii, daima, halihojiwi swali kamwe. Sio karama ya unabii; karama ya unabii inakuwa kwa mmoja, halafu kwa huyo mwengine. Nabii huzaliwa, amekusudiwa tangu zamani na Mungu. Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Mungu aliyechaguliwa tangu zamani. Isaya alimwambia Yohana, Yohana Mbatizaji, miaka mia saba kumi na mbili kabla hajazaliwa, yeye alikuwa ni “sauti ya mtu aliaye nyikani.” Mungu alimwambia Yeremia, “Kabla hata hujaumbwa katika tumbo la mama yako, nilikujua na kukutakasa, na kukuchagua kuwa nabii kwa mataifa.” Na unapowaona manabii wakitokea, hukumu imekaribia.

<sup>209</sup> Sasa, “Hukumu huanza katika Nyumba ya Mungu, kwa watu wa Mungu.” Sasa tumekosea! Tumefanya makosa. Nami ninaamini ya kwamba hao walioketi hapa usiku wa leo, ambao ni Uzao wa Ibrahim na kweli wamechaguliwa kusudi Nuru ya Mungu ipate kuliangazia; wakati Nuru inapolimulikia, wao watasimama. Kuna jambo halina budi kutukia, uko pale! Sasa mko hapa, na tuinamishe vichwa vyetu na kutubu makosa yetu.

<sup>210</sup> Ewe rafiki mwenye dhambi, kama unasimama kwenye kundi hili hapa, ambapo wapo wengine, jionee aibu; bali ni baraka kwako sasa, umelipokea, ukaliamini kwa moyo wako wote.

<sup>211</sup> Enyi Wakristo, enyi wanawake mnaojua, ninaamini ninyi ni wanawake wazuri. Mungu awabariki. Ninaamini jambo hilo. Mungu anaweza kuonyesha hisi ya moyo wangu kwenu. Sitaki kuwa mchoyo kwako dada; nina mke, pia, na wawili—wasichana wawili wadogo. Ninakupenda kama dada yangu.

<sup>212</sup> Na, ndugu, sikutaka kuudhi hisia zenu, lakini wakati mwengine kutikiswa kidogo kwa Neno huwasaidia.

<sup>213</sup> Sasa, kama tumekosea, hebu tuseme tumekosea. Na kuna—kuna neema, kwa wingi sana, kwetu usiku wa leo. “Yeye atakayekiri makosa yake, kuna rehema kwake. Yeye atakayeficha dhambi yake, hatafanikiwa kamwe.” Dhambi yako ni nini? Kutokuamini kwako. Kama ukikuficha, useme, “Vema, mimi ni mzuri tu kama hao wengine.” Umekosea. Wala hutasonga mbele zaidi ya vile unasonga sasa. Utakaa hivyo, hutaenda mbali zaidi mpaka utakapovuka kizuizi hicho na kulisahihisha. Kumbuka, huwezi kufanya jambo hilo; itakubidi kulikanyaga chini Neno la Mungu.

<sup>214</sup> Na mradi tu ungali hai, daima utakumbuka jambo hili. Siku iliyo ndefu sana utakayoishi, utaukumbuka usiku wa leo. Kumbuka, ninakwambia BWANA ASEMA HIVI! Nilikuwa nimeketti mwituni alasiri ya leo, nikiomba. Alinena nami juu ya jambo hili hapa, kasema, “Liseme na ulipazie sauti, nami nitakufanya jambo fulani.” Na ndilo hili hapa.

Sasa na tuombe.

<sup>215</sup> Baba wa Mbinguni, kwa uchaji na uaminifu wenye dhambi wamesimama kwenye kusanyiko hili papa hapa sasa. Wameamka kwenye viti vyao na wakaja hapa, wapate tu kukiri. Wapo Wakristo ambao wamekuja, wakiungama.

<sup>216</sup> Hawa hapa maskini dada wa thamani ambao Nuru imewamulikia, kwenye kilindi cha moyo wao walijua walikuwa wamekosea, walijua ya kwamba Biblia inafundisha mambo hayo, nao wako tayari sasa kuyaacha yote.

<sup>217</sup> Hawa hapa ndugu wamesimama hapa, ndugu wa thamani, wana wa Mungu aliye hai, ambao, kwa kanuni za imani na hali ya uvuguvugu, wametangatanga ulimwenguni. Wanarudi usiku wa leo, Baba. Wanarudi. Wao ni ninii, hawa hapa.

<sup>218</sup> Sasa, Baba, tunatambua ya kwamba wakati waliposimama kwa miguu yao, walivunja; wanasyansi wote, wanasema kwamba huwezi kuinuka, unashikiliwa chini. Bali wakati walipoiuua mikono yao na kuja huku, walithibitisha ya kwamba kulikuwako na Roho fulani ndani yao ambaye angeweza kufanya uamuzi. Wameufanya kwa Kristo.

<sup>219</sup> Yesu, haya hapa Maneno Yako Mwenyewe, nami nitayanukuu tu Kwako.

<sup>220</sup> Ninakupa Wewe watu hawa usiku wa leo, kama mtumishi Wako. Nimefanya kama tu ulivyoniambia nifanye, leo huko mwituni, na hili hapa ndilo hasa ulilosema lingetukia. Na kuna mashahidi wa mambo hayo, wanaosimama hapa. Kuthibitisha Uwepo Wa—Wako, Wewe ulipitia kwenye kusanyiko hili, ukiwaambia hao watu kwamba walikuwa ni akina nani na mahali...wamefanya, na kadhalika, ukiwajua watu hawa, majina, na kwamba walikuwa ni nani na ni mambo gani waliyofanya, shida zao.

<sup>221</sup> Na sasa ulisema katika Neno Lako, ya kwamba, "Yeye atakayenikiri mbele za watu, yeye nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Yeye atakayenionea aibu mbele za watu, yeye nitamwonea aibu mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Sasa hawa dada na hawa ndugu wamesimama usiku wa leo mbele ya wafuasi wao na wachungaji wao, na wapendwa wao, kusema ya kwamba—ya kwamba hawakuonei aibu, bali wanaonea aibu yale wamefanya. Sasa nina hakika, Bwana, ya kwamba Wewe unawasamehe. Uliliahidi. Ulisema, "Yeye atakayekiri dhambi zake, yuna rehema." Nao wanazikiri, nao watapata rehema. Nawe unayeweza kuwaponya wagonjwa, na kusema, "Hivi si ni rahisi vivyo hivyo kusema, 'Umesamehewa dhambi zako,' kama vile kusema 'Chukua kitanda chako na uende'?"

<sup>222</sup> Ninawadai hawa. Ni—ninamundai kila mmoja wao, Bwana. Nimejaribu kukutetea miaka hii yote, na Neno Lako. Nao wamekutetea usiku wa leo, nami ninawadai. Ninawatoa kutoka kwenye mataya ya ulimwengu, nami ninawakabidhi Kwako,

Bwana Yesu. Hao ni vito vya Ujumbe huu usiku wa leo, vya Neno la Mungu. Wadumishe, Mwenyezi Mungu, chini ya Nguvu Zako Takatifu. Naomba wakue, jalia Nuru ya Mungu imulike maishani mwao. Jalia wanaume hao na wanawake, Bwana, waanze kukua katika nguvu na mamlaka ya Roho Mtakatifu. Jalia jambo fulani litukie litakalobadilisha makanisa yao yote na—na ujirani wote mahali walipo. Tujalie, Bwana. Ninawakabidhi Kwako, wao ni Wako. Wao—wao ndio vito vya mkutano huu usiku wa leo, vya Neno lililohubiriwa. Ninayadai maisha yao, katika Jina la Yesu Kristo. Ninataka kukutana nao kwenye ng'ambo ya pili, wakati watakapokuwa wasiopatikana na mauti, wamebadilika wakawa vijana wanaume na wanawake tena, na wakiwa vijana na wa kupendeza milele. Wao ni Wako, Baba. Wao ni vito ambavyo Mungu amempa Mwanawewe, Kristo Yesu, kwa nguvu za Uwepo Wake na Neno la Mungu. Wao ni Wako, Baba. Ninawakabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo; na kudai kila uhai, kila uhai unaosimama hapa. Kila toba imepokelewa, kila dhambi imesamehewa.

<sup>223</sup> Na kila mmoja anayesimama hapa, mimi—mimi—mimi ninaomba nguvu za Roho Mtakatifu ziwe ndani yao, wapate kutekeleza, kufanya yale yaliyo mema, kuwasaidia katika saa hii yenye giza wakati ulimwengu umejaa ubembe. Na, Ee Mungu, nisaidie kesho usiku, ku—kulileta likiwa safi na dhahiri kwao, Bwana; na kukatilia mbali kila vivutio vya ulimwengu huu, wapate kuwa tayari kumlaki Kristo kwenye wakati wa Kuja Kwake. Tujalie, Baba. Tunakuamini sasa.

Na wakati vichwa vyetu vimeinamishwa.

<sup>224</sup> Kila mmoja wenu unayesimama kwa miguu yako, siamini mlikuja kudadisi, kwa kuwa mmekuja chini ya mahubiri makali, magumu ya Injili, yanayokatakata. Lakini mnaamini ya kwamba Yesu alisema kwamba, “Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu, na wote alionipa Baba watakuja.” Sasa hilo ni Neno la Mungu lillothibitishwa. Yeye alimwambia Ibrahimu, Yeye aliahidi na kuapa kwa kiapo, na hapa mliisikia Sauti ya Mungu usiku wa leo na mkaja juu ya misingi hiyo. Hamna budi kusamehewa! Nanyi nyote mnalikubali na kuamini ya kwamba Mungu anawasamehe kosa lenu, na tangu usiku huu na kuendelea, kwa neema ya Mungu, mtamwishia maishani mwenu mwote, na kufanya kila kitu ambacho Biblia hii inawafundisha kufanya, na mwamini kwamba Mungu anawapa neema ya kufanya hivyo sasa, kwa kuwasamehe yaliyopita; inua mkono wako, useme, “Ninaamini kwa moyo wangu wote.” Mungu awabariki.

<sup>225</sup> Nanyi nyote Wakristo huko mliko mnaowajivunia, semenii, “Mungu asifiwe, kwa ajili yao!” [Kusanyiko linasema, “Mungu asifiwe, kwa ajili yao!”—Mh.] Hebu na tuseme tena. Mungu asifiwe, kwa ajili yao! [“Mungu asifiwe, kwa ajili yao!”]

Sasa hebu na tusimame kwa miguu yetu, kila mmoja. Ninataka sauti ya:

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>226</sup> Hebu sote pamoja sasa, kila mmoja aimbe huku tumeinua mikono yetu juu. Vema.

Nampenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>227</sup> Hivi hamjisikii mmesuguliwa kabisa? Hivi Neno la Mungu kwa namna fulani haliwasugui sana na kuwafanya mjisikie vizuri zaidi? Sivyo?

<sup>228</sup> Hamwamini mimi kuwa ni—ni—ni mwongo, sivyo? Mnaamini mimi ni Kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina!”—Mh.]

<sup>229</sup> Ninamwangalia sasa hivi yule Malaika wa Bwana Ambaye mimi humwangalia juu ya watu, amelizungukia kundi hili linalosimama hapa katika umbo la msalaba. Mungu Mbinguni! Picha ile ile ninyi... Malaika mnayemwona kwenye picha ile, yupo papa hapa sasa juu ya kundi hili la watu, akizunguka tu, ninaendelea kumwangalia, kutoka mahali pamoja hadi pengine. Ninaamini, hata, ya kwamba kila maradhi yanayosimama kwenye umati ule yametoweka. Ni—ninaamini hilo kwa moyo wangu wote, ya kwamba kila dhambi imesamehewa.

<sup>230</sup> Hebu na tuninii tu—hebu na tupeane mikono sisi kwa sisi wakati tukiimba “Nampenda.” “Na...” Semeni, “Mungu asifiwe!” [Kusanyiko linasema, “Mungu asifiwe!”—Mh.]

. . . mpenda, nampenda  
Kwani alinipenda kwanza  
Na kununua wokovu wangu  
Mtini Kalvari.

<sup>231</sup> Sasa hebu na tumsifu, tuseme, “Bwana asifiwe! Asante, Bwana Yesu.” Tunakushukuru, Bwana, kwa kuwaingiza watu, kwa ajili ya Neno Lako. Ni kali kama upanga ukatao kuwili, bali linayatambua mawazo ya moyo. Linahakikisha. Linaukatilia mbali ulimwengu, mwili, unayaondolea mbali mambo ya ulimwengu kutoka kwa watu, na kuwafanya viumbe wapya katika Kristo. Jinsi tunavyokushukuru, Baba! Tunakusifu kwa moyo wetu wote. Tunakushukuru kwa ajili yao, Bwana. Jalia wote wajazwe kwa Roho! Jalia Roho Mtakatifu awachukue tu chini ya mamlaka Yake, na jalia uamsho wa mtindo wa kale uibuke mionganini mwa makanisa haya, Bwana, ambao utaenea kote katika jamii hizi, kila mahali pashike moto kwa nguvu za

Mungu. Tutumie pentekoste halisi, Bwana, nguvu halisi za Roho zirudi ndani ya maisha ya watu hawa. Tujalie, Baba.

<sup>232</sup> Hao ni Wako. Kwa neema ya Mungu, hao ni Wako. Hao ni Uzao wa Ibrahimu, kulingana na ahadi. Tujalie, Bwana. Wanaliamini Neno Lako; chochote kinyume, kana kwamba hakikuwako. Wanaamini Neno kwa sababu wao ni Uzao wa Ibrahimu. Wao ni Wako, Baba, kanisa lilidochaguliwa tangu awali lipate kutoa nuru katika siku ya mwisho. Asante, Baba, kwa ajili yao.

Nampenda . . .

Inueni mikono yenu sasa kwa kumsifu Yeye. “Na . . .” Huko juu kabisa kwenye roshani! Hiyo ni kweli.

Kwani alinipenda kwanza na . . .



*YEHOVA-YIRE I* SWA62-0705  
(Jehovah-Jireh !)  
MFULULIZO WA YEHOVA-YIRE

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ultolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 5 Julai, 1962, katika Ukumbi wa Manispaa huko Grass Valley, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## **Ilani ya haki ya kunakili**

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

**VOICE OF GOD RECORDINGS**  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)